# Nipashe

Jumatano Juni 24, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580266

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

• Jifunze kuhusu Ualbino

• Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN

The Global Religions for Children Foundation




## Mjamzito apata uchungu mahabusu, afariki dunia

UKURASA 4

# IGP Sirro: Tunamsubiri kwa hamu Tundu Lissu




IGP Simon Sirro

Tundu Lissu

## Membe ataja mpango kuwania urais upinzani

UKURASA 4

## ZITTO APATA DAWA YA KUKWEPA 'FIGISU' ZA UCHAGUZI

UKURASA 3

### BAA LA CORONA



Mtu anaweza kupata maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 kutoka kwa mwingine kupitia majimaji yanayotoka kwenye pua au mdomo wa mtu mwenye ugonjwa huo. Tafadhali jikinge kwa kuvaa barakoa kwenye mkusanyiko wa watu. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO SIMBA, YANGA MAJARIBUNI BARA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# IGP Sirro: Tunamsubiri kwa hamu Tundu Lissu

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi nchini, limesema linamsubiri kwa hamu Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ili limhoji kupata ushahidi wa tukio la kushambuliwa kwake.

Akizungumza katika kipindi cha Dakika 45 cha ITV juzi usiku, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, alisema tangu awali, tukio la kushambuliwa Lissu lilikosa ushirikiano wa ushahidi.

"Suala la Lissu ushirikiano ulikuwa hakuna kabisa na lilichangia upelelezi wetu kuwa mgumu. Hata dereva wake tulipokwenda kumhoji, hakutaka kuonyesha ushirikiano kwa Jeshi la Polisi.

"Wewe umeshuhudia tukio, halafu polisi wamekuja kukuhoji, hutaki hata kuwapa fursa ya kutaka wakuone, hapo sasa unategemea polisi watafanya nini?" alihoji.

IGP Sirro alisema hata kama Lissu akiishi Ulaya na kurudi Tanzania baada ya miaka 20, lazima Jeshi la Polisi litamhoji tu kuhusu tukio la kushambuliwa kwake.

"Sasa ninashukuru kwamba kwa vile anagombea urais, na kama atapewa nafasi na chama chake, ninafikiri atakuja nchini na tutamhoji vizuri tupate maelezo yake kwa sababu upelelezi au tukio huwa halifiki mahala likawa mwisho.

"Hata kama angekaa Ulaya miaka 20, akija bado tutamhoji kujua ukweli wa jambo. Lakini kwa vile anakuja, niombe aje, maana yake nina haja sana ya kutaka kuja kumhoji, ili kujua ukweli wa jambo lenyewe likoje," alisema.

IGP Sirro alisema upelelezi ni suala mtambuko na kwamba wakati mwingine umekuwa ukichelewa zaidi kwa sababu lazima ushirikishe mamlaka nyingine.

"Sula la upelelezi ni mtambuka, kwa sababu mfano mtu amekufa, ni lazima ushirikishe Mkemia Mkuu wa Serikali, madaktari, kwenye tukio umeona kitu gani?

"Kwa hiyo, siyo suala la mara moja unapata majibu au ushahidi wa kuthibitisha kosa. Wakati mwingine inategemea na ugumu wa tukio lenyewe," alifafanua.

Alikiri kuwapo kwa baadhi ya matukio ambayo ushahidi wa kutosha umekuwa ukikosekana na yamekuwa yakiondolewa kwenye uchunguzi wao, lakini kwa matukio makubwa, likiwamo la Lissu, si rahisi kuyaondoa.

"Kwa mfano suala la Tundu Lissu bado hatujapata maelezo yake, tunalifungaje hilo jalada? Ni lazima tumsubiri tupate maelezo yake ili tuone kama kuna vitu anaweza kutusaidia kupata majibu ya malalamiko yake," alisema.

Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risali katika sehemu mbalimbali ya mwili wake Septemba 7, 2017 mchana alipokuwa anajiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake jijini Dodoma muda mfupi baada ya kumalizika kwa kikao cha Bunge, ambacho pia alishiriki kuchangia hoja.

**MBOWE KUSHTAKIWA?**

Akizungumzia madai ya kushambuliwa kwa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, IGP Sirro alisema bado uchunguzi wake unaendelea na kwamba endapo watabaini kwamba taarifa zilizotolewa ni za uongo, watampeleka mahakamani.

"Suala la Mbowe tunaendelea kuchunguza, nilitoa maelekezo tupate ushahidi maana ushahidi namba moja siku zote ni kwenye eneo la tukio. Sasa kama eneo la tukio ushahidi hakuna na kila mtu anasema hajasikia... hajasikia.... hajasikia! Sitaki nimhukumu mtu, lakini upelelezi unaendelea.

"Ila ninataka Watanzania waelewe kwamba tukibaini kuna taarifa ya uongo, ninarudia... tukibaini kuna tarifa ya uongo, hakuna mtu aliye juu ya sheria, tutampeleka mahakamani kwa kutoa taarifa ya uongo," alisisitiza.

IGP Sirro pia alikiri Jeshi la Polisi kulazimika kutumia nguvu ya ziada kumhoji dereva wa Mbowe, akifafanua: "Kwa mfano, wakati tunajaribu kumhoji dereva wake, alizuiwa asiseme chochote na ilibidi tutumie nguvu ili aseme chochote. Kwa mazingira hayo, inakuwa na mashaka makubwa sana."

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi aliongeza: "Mtu anaposhambuliwa ni lazima tupeleleze, ili tujue -- je, ni kweli kashambuliwa? Kwa sababu si kila taarifa huwa ni sahihi."

Mbowe alidaiwa kushambuliwa Juni 8, mwaka huu na watu wasiojulikana nyumbani kwake jijini Dodoma na kulazimika kukimbizwa katika kituo cha afya jijini huko kisha kuhamishiwa jijini Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu zaidi.

**UCHAGUZI MKUU**

Akizungumzia Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, IGP Sirro alisema wamejipanga kuhakikisha unafanyika katika hali ya amani na usalama na hawatamvumilia mwanasiasa yeyote atakayejaribu kuchochea vurugu.

"Kuelekea Uchaguzi Mkuu, tumejipanga vizuri, hata kama ungefanyika leo. Sisi wenyewe ndani tunapeana elimu kwa sababu unaposimamia kanuni au sheria ni lazima uzijue.

"Wakati wa uchaguzi kuna kanuni na taratibu zake, sasa wakati wa uchaguzi lazima kila kinachofanyika kiwe ni halali na kama si halali ni kuvunja sheria na huwezi kuachwa.

"Kama ni maandamano, kuna utaratibu wake na lazima ufuatwe na kama hujafuata utaratibu, unakuwa umevunja sheria na umekuwa mhalifu," alifafanua.

Alitahadharisha makundi ya watu ambao hufanya vurugu katika vituo vya kupigia kura kwa madai ya kulinda kura, akisisitiza kuwa hawatawavumilia.

"Hayo mamlaka ya kulinda kura wameyapata wapi? Na kama hakuna kanuni ambayo imetoa mamlaka ya kulinda kura, maana yake unavunja sheria na ukivunja sheria, tutakushughulikia kwa mujibu wa sheria ile ambayo umeivunja wewe.

"Niwaambie Watanzania kwamba taratibu zipo, mahakama zipo, ukiona hujaridhika, utaenda mahakamani, lakini suala la kuamua kuvunja sheria, ninasikitika sana kwamba mwishowe utajialaumu kwa sababu utakuwa umetaka mwenyewe.

"Nilisikia kiongozi mmoja anasema damu itamwagika, mimi nilisikitika sana, unataka kuwa kiongozi, lakini unataka watu wamwage damu. Imwagike ya Watanzania au imwagike ya kwako?

"Kabla hujasema jambo, unatakiwa ulifikirie mara mbili kwamba unasema hayo kwa faida ya nani? Je, hiyo damu inamwagika, serikali ipo au haipo?

"Kama serikali ipo, maana yake suala la damu kumwagika halipo na kwa bahati nzuri Watanzania wengi hawapendi kumwaga damu kwa sababu ya uchaguzi.

"Niwaombe sana hii mihemko mingine haina tija, kama kuna jambo halijaenda vizuri, wafuate taratibu, wasijiingize kwenye uhalifu kwa sababu tutakumbana tu.

"Mimi nipo, vyombo vipo, jeshi lipo, hatutakuacha, yaani kwa sababu ya 'interest' (maslahi) yako wewe mtu mmoja, ufanye watu wafe?" alionya.

IGP Sirro pia alizungumzia kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa na hadhara, akisema kufanyika kwake kuna taratibu zake ambazo lazima zifuatwe.



Mtiania nafasi ya urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Zanzibar, Mohammed Hija Mohammed (kulia), akirejesha fomu kwa Katibu wa Kamati Maalumu ya Idara ya Oganaizesheni ya CCM, Cassian Gallos Nyimbo, katika Ofisi za CCM Kisiwandui mjini Unguja, jana. **PICHA: MUHIDIN SUFIANI.**

## Mchezaji soka awa wa 24 CCM kutia nia urais Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Zanzibar, Salum Hashim Salum, amechukua fomu kuomba ridhaa kuteuliwa kuwania urais wa Zanzibar mwaka huu kupitia chama hicho.

Hashim anakuwa kada wa 24 kuchukua fomu katika Idara ya Oganaizesheni ya chama hicho na kutakiwa kutafuta wadhamini 250 katika mikoa mitano ya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuchukua fomu hiyo, Hashim alisema akichaguliwa, anakusudia kutoa kipaumbele kwa sekta ya michezo nchini.

"Mimi ni mchezaji wa soka wa zamani na kiongozi wa mpira wa miguu, ukiacha mambo ya siasa, ninakusudia kuimarisha soka ili kutoa ajira kwa kundi la vijana nchini," alisema.

**WAREJESHA FOMU**

Wakati Hashim akichukua fomu, makada watatu kati ya 24 waliojitokeza kuomba kupewa ridhaa ya chama kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar, wamerudisha fomu hizo.

Makada hao ni Balozi Ali Abeid Karume, Balozi Mohammed Hija Mohammed na Mbwana Bakari Juma ambao wametimiza masharti ya kutafuta wadhamini 250 katika mikoa mitatu ya Zanzibar.

Wagombea 24 waliokuwa wamechukua fomu hadi jana ni pamoja na: Mbwana Bakari; Balozi Ali Karume; Mbwana Mwinyi Yahya; Omar Shehe; Muhammed Jafar; Muhammed Hija; Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor; Shamsi Vuai Nahodha; Dk. Hussein Mwinyi; Profesa Makame Mbarawa; Mwatum Mussa Sultan; Haji Rashid Pandu; Dk. Abdulhalim Mohammed Ali; Jecha Salim Jecha; na Dk. Khalid Salum Muhamed.

Wengine ni: Rashid Ali Juma; Khamis Mussa; Mmanga Mjengo Mjawiri; Hamad Yussuf Masauni; Muhammed Aboud; Bakari Rahid; Ibrahim Makungu; Ayoub Muhammed Mahmoud; na Hashim Salum Hashim.

## HABARI KITAIFA

# Wanne akiwamo askari polisi mbaroni tuhuma za mauaji

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

POLISI mkoani hapa inawashikilia watuhumiwa wanne akiwamo askari polisi kwa tuhuma za kumuua dereva bodaboda Erasto Mwalwego (29), mkazi wa Nzovwe.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, miongoni mwa watuhumiwa hao ni askari wa polisi John Kaijage (34), mkazi wa Isyesye.

Aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Fotunatus Kagande (23), Petson Daniel (22) na Jastini Kagande (27), ambaye ni mwanafunzi.

Alisema tukio hilo la mauaji lilifanyika Juni 20, saa tatu usiku katika nyumba ya kulala wageni iliyopo Iwambi baada ya watuhumiwa kumshambulia Mwalwego kwa kitu butu.

Alisema Malwego alipelekwa Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya kwa matibabu na Juni 21 alifariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

"Jeshi la Polisi tunaendelea na upelelezi kubaini chanzo cha mauaji haya ya kijana Erasto Mwalwego dereva bodaboda na baada ya kukamilika shauri litapelekwa mahakamani ili watuhumiwa kujibu tuhuma za kuhusika na tukio hilo," alisema Matei.

Katika tukio lingine polisi imemkamata Bahati Ndinagwe, mkazi wa Kijiji cha Kilwa, Kata ya Kajunjumele, wilayani Kyela kwa tuhuma za kughushi nyaraka za serikali ambayo ni barua inayoonyesha kuwa imetoka Ofisi ya Usalama wa Taifa makao makuu kwenda kwa mtuhumiwa huyo ikimjulisha kuwa ameteuliwa kujiunga na Idara hiyo ya Usalama wa Taifa.

Matei alisema barua hiyo ilieleza kuwa lengo lilikuwa ni kupata ajira huku akihitaji kuchapa barua hiyo kwa namna inayofanana na barua za Idara za Uhamiaji ili apate ajira.

# Zitto apata dawa kukwepa ya uchaguzi serikali mitaa

**Na Enock Charles,** RUFIJI



Mafundi wa kampuni ya China Railway Group, wakiendelea na ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua katika eneo la Chang'ombe Kibasila, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema watahakikisha wanaandaa wagombea na kuwapa maelekezo vizuri namna ya kujaza fomu, ili kusijitokeze kile alichokiita visingizio vya tume kukata majina yao kama ilivyokuwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Akizungumza na wananchi katika Jimbo la Rufiji mkoani Pwani juzi, Zitto alisema watahakikisha wagombea wao wote wanapata maelekezo maalum ya kujaza fomu hizo.

Alisema kuwa kabla ya kujaza fomu hizo, wagombea wao watapata msaada wa mawakili wa vyama, lengo likiwa ni kukwepa kilichotokea dhidi ya wagombea wa upinzani katika uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Novemba mwaka jana, baadhi ya vyama vya upinzani, vililazimika kujitoa kwa madai ya kuchezwa rafu kwa wagombea wake wengi kuenguliwa kutokana na madai ya kutojaza fomu kwa umakini na kushindwa kurejesha fomu baada ya wasimamizi wa uchaguzi kuamua makusudi kufunga ofisi.

Zitto pia alisema kuwa vyama makini vya upinzani havina mpango wa kususa kushiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, lakini vitaendelea kudai tume huru ya uchaguzi.

"Tujipange kufanya mabadiliko ya kisiasa nchini, ninajua tuna hofu lakini tuondoe hofu tupambane, hakuna njia nyingine ya kumwambia mtawala kuwa tumekasirika ila kwa karatasi ya kura," Zitto alisema.

Katika ziara hiyo jimboni Rufiji, Zitto alipokea wanachama wapya waliohamia katika chama hicho kutoka vyama vingine, akitamba kuwa tayari chama chake kimeshafanya maandalizi yote muhimu kuelekea uchaguzi huo na kuwaomba wananchi hao kuwa tayari kushiriki katika uchaguzi na kukiunga mkono.

Viongozi waliwapokewa juzi na Zitto katika ziara yake hiyo ni pamoja na madiwani wanne ambao ni: Juma Mlanzi kutoka Kata ya Umwe; Issa Miduma (Kipugila); Hassan Mpota (Mgomba); na Sofia Mkengesi (Viti Maalum), wote kutoka Chama cha Wananchi (CUF).

Kuhusu ushirikiano wa vyama katika uchaguzi huo, Zitto alisema ni muhimu kwa vyama makini kushirikiana katika uchaguzi huo, ili kupata nguvu ya pamoja kuking'oa Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani.

Zitto alisema kuwa asilimia kubwa ya wananchi wanaotegemea kilimo, bado ni maskini kutokana na kutotengewa fedha za kutosha katika bajeti ya serikali ya kila mwaka katika kipindi cha awamu ya kwanza cha serikali ya awamu ya tano, huku fedha nyingi zikielekezwa katika sekta ambazo haziwasaidii wananchi wa hali ya chini.

"Katika kila Watanzania 100, Watanzania 67 wanategemea kilimo, lakini kilimo kimetengewa asilimia 0.6 ya matumizi yote ya serikali huku fedha nyingi zikipelekwa katika ununuzi wa ndege," Zitto alilalamika.

Aliongeza kuwa mwaka huu hawatakubali kuporwa ushindi visiwani Zanzibar, akidai kuwa kwa miaka yote ambayo Mwenyekiti wa chama hicho, Maalim Seif Sharrif Hamad, ameshiriki, amekuwa akiporwa ushindi wake.

# Baba mzazi atuhumiwa kumbaka mwanawe, amtongoza kwa 5,000/-

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

BABA mmoja anatafutwa na polisi wilayani Bunda, kwa tuhuma za kubaka mtoto wake wa kumzaa mwanafunzi wa darasa la saba.

Akisimulia tukio hilo juzi mbele ya Mkuu wa wilaya hiyo, Lydia Bupilipili, Mkuu wa kituo cha polisi Nyamuswa, Simon Joseph, alisema mtu huyo (jina tunalo), anatuhumiwa kumbaka mtoto wake hivi karibuni nyumbani kwake usiku katika kijiji cha Nyamuswa.

Akisimulia tukio hilo mwanafunzi huyo, alisema baba yake alianza kumtongoza huku akisema kuwa atampatia Sh. 5,000 na baada ya kumkatalia, usiku alimvamia ndani ya chumba chake na kumkamata kwa nguvu akiwa amemziba mdomo kwa mikono yake.

Mwanafunzi huyo alisema kuwa hiyo ilikuwa ni mara ya pili baba yake kumfanyia ukatili huo na kwamba siku hiyo ya pili baada ya kufanyiwa unyama huo alikimbia na kupiga yowe na shangazi yake alifika na kumchukua na kumlazimisha kujisafisha sehemu za siri ili asionekane kama amebakwa.

"Hii ni mara ya pili baba ananibaka, siku ya kwanza alinifanyia hivyo akaniambia kwamba kama nikisema sehemu yoyote ataniua. Sasa ile siku ya pili aliniambia kwamba anipe shilingi elfu tano tulale naye mimi nikamwambia kuwa si ni baba yangu, lakini usiku akanigongea mlango eti akiomba maji ya kunywa.

"Mimi nikamwambia baba si maji unayo huko akanilazimisha ndipo nikafungua mlango na kumpatia maji nilivyotaka kufunga mlango akaweka mkono wake nikashindwa kuufunga ndipo aliponivamia kwa nguvu na kunifanya kitendo hicho," alisema mwanafunzi huyo.


EXCAVATORS FOR SALE

effco
Plant & Crane Hire

EFFCO SOLUTIONS (T) LTD

Is calling for serious buyers to purchase its three (3) Excavators as detailed below






MAKE : Caterpillar

MODEL : 320D

Year : 2010

For pricing and more details call seller
+255752330590 OR +255762209081

115787702

# Membe ataja mpango kuwania urais upinzani

**Na Mary Geofrey**

ALIYEWAHI kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Benard Membe, ameendelea kutia mkazo mpango wake wa kuwania urais kupitia chama chochote cha siasa nchini.

Membe ambaye mwaka 2015 alitia nia kuwania urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), amesema kama chama chake hicho kitamsafisha kuhusu tuhuma zinazomkabili, atachukua fomu ya kuwania nafasi hiyo.

Membe alivuliwa uanachama na Kamati ya Maadili ya CCM, Februari mwaka huu, baada ya sauti yake na makada wengine wa chama hicho kuvuja kwenye mitandao ya kijamii, wakielezea namna chama hicho kilivyokosa mwelekeo.

Katika tukio hilo, makada wenzake waliomba msamaha kwenye chama na kusamehewa, hata hivyo Membe ameendelea kusisitiza chama hicho kilimkosea na ana matumaini kitamsafisha.

Alitangaza msimamo wake huo kupitia mahojiano maalum na Idhaa ya Kiswahili ya DW, kijijini kwake Londo, mkoani Lindi na kurushwa jana.

Membe alisema CCM kikimsafisha, ni wazi kuwa atawania urais kupitia chama hicho kwa sababu ni haki yake ya kikatiba kufanya hivyo na kwamba siyo dhambi kugombea.

"Ni kweli kabisa mwaka huu nitagombea, lakini sijui nitagombea kupitia chama gani kwa sababu moja kama CCM 'itani-clear' (itanisafisha), ninaweza kugombea kupitia CCM kwa sababu ni haki yangu na furaha yangu ni furaha ya watu pia kuona watu wakishindana na wala siyo dhambi kugombea.

"Nami ninaomba kutumia fursa hii kuwaambia upinzani, wasije wakadhani kuwa ni dhambi kupambana na Rais aliyepo madarakani, ukidhani ni dhambi, ni ujinga, hii ni haki yako ya kikatiba, unayo haki ya kuchagua, unayo haki ya kuchaguliwa," alisistiza Membe.

Kuhusu kupitishwa na chama hicho, alisema anaweza asiwe na nafasi ya kupitishwa, lakini anaweza kuwa na haki.

Membe alisema ana uhuru wa kugombea kupitia chama kingine cha siasa kwa sababu kukosa haki ndani ya chama, kunampa uhuru kutafuta haki kupitia chama kingine.

Alisema siyo lazima kuwania nafasi ya urais kupitia chama cha ACT-Wazalendo wala Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) isipokuwa chama chochote kitakachompendeza anaweza kutumia kuwania nafasi hiyo.

"Mimi ninakuambia uwanja upo mezani, chochote kinaweza kuja kitakachonipendeza ninaweza kufika," alisema Membe.

Alisema yeye pamoja na wanachama wengine sita wa CCM wana msimamo kama wake, lakini hawezi kuwataja kwa sasa kwa sababu wanaweza kufukuzwa chama wakati wowote kuanzia sasa.

"Siwezi kuwasema kwa sababu watafukuzwa chama, nakuapia leo kama tusingekuwa tunafukuzana, ningekupa majina yote sita mimi wa saba, lakini watafukuzwa kesho asubuhi," alisema.

Alisema kuwa tangu mwaka 2015, amekuwa akishambuliwa kuwa anamshambulia Rais na serikali iliyopo madarakani na anatembea kukusanya fedha kwa ajili ya kuwania urais mwaka 2020.

Alisema tuhuma hizo siyo za kweli na hata kamati ya maadili ya CCM ilishindwa kuzithibitisha.

Kuhusu makosa yake ya kuvuja kwa sauti, alisema suala hilo siyo kosa la kujutia, bali jambo kubwa lililompeleka Kamati Kuu ni kudukuliwa ambalo ni kosa la jinai kwa mujibu wa Katiba ya nchi kifungu cha 8 C.

"Kwa hiyo, wewe uliyenidukua huwezi kuniambia mimi nikuombe radhi baada ya kunidukua, wewe uliyenidukua unatakiwa uniambie nani alikusaidia kunidukua, nikujue nikuchukulie hatua kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu," alisema Membe.

Kadhalika, Membe alisema kwenye Kamati ya Maadili aliuliza nani alimdukua, lakini hakupata jibu.

"Niliwabana kweli pale 'ni nani aliyenidukua ili nimchukulie hatua kama ninyi mnavyotaka kunichukulia hatua'," alisema.

Kuhusu wasiwasi wake wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), alisema siyo tume huru ya uchaguzi kwa sababu hakuna neno huru kama zilivyo tume nyingine za uchaguzi duniani.



Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Mashariki, Arnold Mapinduzi (kushoto), akiwa na watumishi wenzake, wakifanya usafi kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi, eneo la Daraja la Selander, jijini Dar es Salaam jana, kuadhimisha Siku ya Utumishi wa Umma Afrika.. **PICHA: MIRAJI MSALA .**

## Mjamzito apata uchungu mahabusu, afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

ANASTAZIA Mwahaiki, amefariki dunia wakati akijifungua baada ya kupata uchungu akiwa mahabusu kutokana na kukamatwa Ukonga, Mombasa jijini Dar es Salaam na kuzuiwa kwa saa nane ndani ya ofisi za kata kwa madai ya kushindwa kulipa fedha za taka.

Mume wake, Walter Kihonga, ambaye ameachiwa watoto wawili, kikiwamo kichanga alichojifungua mke wake kabla ya umauti, alisema kuwa akiwa kazini, alipigiwa simu kuhusu mkasa huo.

Alisema anajishughulisha na uendeshaji wa trekta la takataka maeneo ya Segerea ambalo kwa muda halifanyi kazi kutokana na kuharibika.

"Nikiwa ninaendelea na shughuli, mke wangu alinipigia simu kunijulisha kuwa mgambo wamefika nyumbani na kuwachukua pamoja na mtoto wao mwingine na kupelekwa ofisi ya kata.

"Mke wangu alinijulisha kuwa watamwachia endapo nitakwenda, lakini alipoazima Sh. 5,000 wakamwachia, wakati akiniambia hayo, nilikuwa bado sijapata fedha," alisimulia.

Alisema awali walishindwa kulipa taka kwa muda wa miezi miwili, hivyo wakawa wanadaiwa Sh. 6,000 na ikaongezeka mingine miwili hivyo jumla ikawa Sh. 12,000.

"Hata mwenye nyumba ananivumilia maana nilimweleza kuhusu hali tunayopitia baada ya trekta kuharibika, niliona niendelee na 'deiwaka' ili nipate fedha za kulisha familia, ningeacha tungekosa hata fedha ya chakula," alisema.

Alisema baada ya mke wake kuachiwa, walimtaka aende ofisi za kata lakini hakufanya hivyo kwa sababu alikuwa hajapata fedha za kulipa.

"Nilimwambia mke wangu wakirudi tena awaambie bado hatujapata fedha za kulipa, sijui ilikuaje tena maana sikupata hata muda wa kumuuliza.

"Aliniambia alikwenda kwa sababu walikuwa na barua ya wito, hivyo baada ya kufika wakamkalisha huko ndipo alipoanza kuumwa uchungu na kumruhusu arudi nyumbani.

"Nilishindwa kumhoji zaidi kwa sababu alikuwa tayari kwenye hali mbaya, tulichukua bajaj tukaenda hospitali ya Pugu, lakini walituambia hawawezi kufanya upasuaji, tukaenda hospitali ya Kisarawe akafanyiwa upasuaji, lakini alifariki na kuniachia mtoto wa kike," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mwembe Madafu, Mbaraka Mohamed, alisema tatizo kubwa ni ukosefu wa ada ya kulipa taka.

Alisema taarifa za msiba huo alipokea juzi zikieleza kuwa mama mjamzito alichukuliwa na mgambo na watu wa afya na kupelekwa kata na kukaa saa nane na alipopata uchungu aliruhusiwa kurudi nyumbani.

"Ni kweli nimekuwa nikipokea malalamiko na nimekuwa nikiwasiliana na mkandarasi mwenye dhamana ya kubeba taka na nilishamjulisha wakifika kwa mtu kudai fedha, basi wawe wapole, wakikosa, basi wawe wavumilivu," alisema.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Mwembe Madafu, Abdallah Mlanzi, ambaye pia yupo kwenye kamati ya afya na mazingira, alisema watu hao ni tatizo na wanapomkamata mtu, 'anakuwa zaidi ya jambazi'.

"Huyu mama mjamzito, ujauzito ni alama ya utu wako, hata akiwa kwenye daladala unatakiwa umpishe akae, sasa unamweka chini ya ulinzi, inasemekana huyu mama amekaa saa nane pale, baada ya kukosa wanachotaka ndipo wakamruhusu huku hali yake imeshaanza kuwa mbaya," alidai.

Nipashe ilipomtafuta Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ilala, ili kuzungumzia tukio hilo, simu yake ilikuwa inaita bila kupokewa.

# Adaiwa kuiba mtoto, achoma godoro ionekane kateketea

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linamshikilia mwanamke mmoja (jina limehifadhiwa), mkazi wa kijiji cha Msata mkoani Pwani, kwa tuhuma za kumuiba mtoto mwenye umri wa wiki moja na kisha kuchoma godoro alilokuwa amelalia mtoto huyo ili ijulikane ameteketea kwa moto.

Tukio hilo lilitokea Juni 11, majira ya saa 2:30 usiku katika eneo la Namanyere, wilayani Nkasi baada ya mtuhumiwa huyo kumuiba mtoto huyo kwa ndugu yake Samia Ruhusa (35), mkazi wa Namanyere wilayani humo.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, alisema siku ya tukio mtuhumiwa alimpigia simu mama wa mtoto huyo na kumwambia kuwa yupo jijini Dar es Salaam, amemtumia fedha za matumizi kupitia mtandao wa simu, aende akazitoe usiku huo ili zimsaidie katika kipindi ambacho amejifungua.

Baada ya mama wa mtoto kuambiwa hivyo aliondoka nyumbani kwake na kumuacha mtoto amemlaza kwenye godoro, ndipo mtuhumiwa anayedaiwa kuwa alikuwa karibu na nyumba hiyo amejificha, aliingia ndani na kuchoma moto godoro alilokuwa amelalia mtoto huyo kwa lengo la kupoteza ushahidi ili idhaniwe kuwa mtoto huyo ameteketea kwa moto na kisha kumchukua na kutokomea naye.

Mama mwenye mtoto aliporudi nyumbani alikuta moto unawake ndani na kuanza kupiga kelele za kuomba msaada, majirani walifanikiwa kuingia ndani na kuuzima moto huo, lakini hawakukuta mwili wa mtoto huyo zaidi ya kukuta kipande cha godoro kikiwa kimeungua.

Kamanda Masejo alisema, mama huyo pamoja na majirani waliamua kwenda polisi kutoa taarifa ya tukio hilo na polisi walianza uchunguzi kwa kuwakamata watu mbalimbali wanaodhaniwa kuhusika katika tukio hilo.

Alisema polisi kwa kushirikiana na wananchi walifanikiwa kumkamata mama huyo akiwa mkoani Pwani, Kijiji cha Msata na alipohojiwa alikiri kufanya tukio hilo la kumuiba mtoto na kutoroka naye, kwa kuwa ametafuta mtoto kwa muda mrefu bila mafanikio ndiyo maana aliamua kwenda kumuiba mtoto huyo wa ndugu yake baada ya kupata taarifa kuwa amejifungua.

Kamanda alisema mtuhumiwa anashikiliwa na polisi na taratibu za kisheria zinafanyika ili afikishwe mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

## Mume aua mke kisha ajinyonga

**Na Ndalike Sonda,**

KAHAMA

WATU wawili ambao ni mume na mke wakazi wa Kijiji na Kata ya Igunda Tarafa ya Dakama Wilaya ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamefariki dunia baada ya kuzuka ugomvi unaoelezwa kutokana na wivu wa kimapenzi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa Mkoa wa Shinyanga ACP Joseph Paul, kwa vyombo vya habari, mwanamke, Christina Jakobo (41), akiwa chumbani, aliuawa kwa kukatwa na panga kichwani na shingoni na mumewe John Chumila (42).

Alisema baada ya tukio hilo, mwanaume huyo na yeye alijinyonga kwa kutumia kamba ya katani juu ya kenchi chumbani humo.

Kamanda Paul alisema kuwa tukio hilo lilitokea Juni 21, mwaka huu majira ya saa 3:00 usiku, na kuwa mauaji hayo yaliyotokea chumbani, yalisababishwa na kinachodaiwa ni wivu wa mapenzi.

Aliongeza kuwa mume alidai kugundua kuwa mke wake anatoka nje ya ndoa.

Alieleza kuwa wanandoa hao walikutwa wamejifungia chumbani, na kwamba miili yao imekabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi.

Kaimu kamanda alitoa wito kwa wanandoa kuacha tabia za kujichukulia sheria mikononi.

Aidha, aliwataka kufuata taratibu za kuwapeleka wenza wao kwenye madawati yaliyopo ofisi za ustawi wa jamii pamoja na vituo vya polisi ili kupata ufumbuzi wapatapo matatizo katika ndoa zao.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (kulia), akikabidhi zawadi ya picha ya Sokwe Mtu kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Balozi John Kijazi, kwa niaba ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), baada ya kuzindua Kivuko cha Kisiwa cha Rubondo pamoja na utalii wa Sokwe, kisiwani humo, mkoani Geita, juzi. **PICHA: WMU**.

# Vijana waitaka Tanzania kuridhia mkataba wa ACDEG

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

JUMUIYA ya Vijana ya Pemba Youth Voice Organization iliyopo chini ya Shirika la Actionaid imeishauri Serikali ya Tanzania, kuuridhia na kuusaini mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora (ACDEG), ili kuiletea nchi maendeleo zaidi.

Walisema mkataba huo ulipitishwa Januari 30, 2007 na kuanza kufanya kazi Februari 12, 2012, ingawa Tanzania haijaridhia wala kusaini, licha ya kuwa ni moja ya mwanachama wa Umoja wa Afrika (AU) ikizingatia kuwa imekuwa ni alama ya amani na utulivu.

Wakizungumza katika mkutano wa vijana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika ukumbi wa Baraza hilo Wete, walisema mkataba huo umekusudia ahadi za wakuu wa nchi za AU kuhusu kuhimiza na kulinda demokrasia, haki za binadamu na utawala wa sheria.

Walisema vifungu vingi vilivyomo pia vipo kwenye mfumo wa sheria za Tanzania, ambapo inaamini utawala wa sheria, demokrasia, utawala bora na haki za binadamu, hivyo ipo haja ya kuridhia na kusaini mkataba huo.

"Kwa mfano suala muhimu la utawala wa sheria linalindwa vizuri na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haki nyingi za kijamii na kisiasa zinalindwa na Ibara ya 12 hadi 29, masuala muhimu ya utawala bora yameainishwa kwenye Ibara za 4, 21 (1), 46 (2), 46 A na 56, Katiba na kanuni za demokrasia kwenye Ibara za 5, 8, 20 na 21," alisema mmoja wa vijana hao.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana, Mohamed Hassan Juma, alisema una ibara 53 ambapo sehemu kubwa inajadili misingi ya muhimu kwenye vifungu vya kanuni za demokrasia, haki za binadamu, utawala wa sheria, ukuu wa Katiba na mpangilio wake.

Aidha, mabadiliko ya demokrasia ya Serikali, utulivu, amani, ulinzi, uhuru wa mahakama, utawala bora, vyama vingi na kuvumiliana, vita dhidi ya rushwa, ushirikishwaji, uwazi, uwajibikaji, usawa wa kijinsia na ushirikiano wa pamoja.

Zamzam Ali Hassan na Hamad Suleiman Hamad, waliiomba Tanzania iridhie mkataba huo kwani italeta maendeleo endelevu kwa vijana na nchi kwa ujumla.

Nao Bimvua Suleiman Ame na Rahima Omar Ali, walieleza kuwa kijana ana nafasi kubwa ya kuendeleza demokrasia, hivyo elimu inahitajika zaidi ili kujielewa na kujua haki zao za msingi, jambo ambalo lisaidia kuleta maendeleo zaidi.

Mkuu wa Idara ya Programu za Sera kutoka Shirika la Actionaid, Jovina Nawenzake, aliwaomba wawakilishi kuusoma kwa kina mkataba huo na kupendekeza usainiwe ili kuonyesha umoja na mshikamano na mataifa mengine.

"Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba Tanzania haijasaini wala kuridhia mkataba huu tokea mwaka 2007, suala hili linaleta hoja hasa ukizingatia Tanzania imekuwa kitovu cha amani na utulivu, hivyo tunaomba kuridhia na kusaini ili kuwaletea vijana maendeleo," alisema.

Mwakilishi kutoka Jimbo la Micheweni Shamata Shaame Khamis, alisema kuwa, kila jambo linakwenda kwa utaratibu wake na maslahi ya taifa, hivyo maombi yao watayapeleka sehemu husika, ili kufanyiwa kazi.

"Naishukuru Serikali namna inavyotekeleza misingi ya demokrasia na Utawala bora, inapiga vita vitendo vya rushwa, hivyo tutalifikisha na iwapo italiona kwamba linafaa na kuwa na maslahi na nchi yetu naamini Tanzania itaridhia mkataba huu," alisema.

"Serikali haiwatakii mabaya wananchi wake pamoja na kuwa mambo yaliyoainishwa kwenye mkataba huu ndio yale yale yaliyomo katika katiba yetu, lakini hatuwezi kujua, inawezekana kuna changamoto ndani yake," alisema Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid.

Katika hatua nyengine mwakilishi wa vijana Mkoa wa Kaskazini Pemba, Viwe Khamis Abdalla , aliwataka vijana hao wasiwe tayari kutumiliwa vibaya na mtu yeyote asiependelea mema nchi yake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kupatikana hati ardhi h'shauri habari njema

**JUZI** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliagiza kutolewa kwa hati miliki ya ardhi ndani ya wiki moja, baada ya mwananchi kukamilisha taratibu zote muhimu.

Waziri huyo alisema hati hizo zinapaswa kutolewa kwenye halmashauri ambazo wananchi wamelipia gharama za kupatiwa hati, ili kuondoa usumbufu na gharama kufuatilia hati kwenye ofisi za ardhi za mikoa.

Waziri Lukuvi aliongeza kuwa tangu kufunguliwa kwa ofisi mpya ya ardhi mkoa wa Tanga, hati zaidi ya 300 zimeandikwa na kusajiliwa kwenye mkoa na kusisitiza kuwa, uanzishwaji ofisi za ardhi kwenye mikoa siyo tu utaondoa usumbufu wa kufuatilia hati bali utapunguza pia migogoro ya ardhi.

Kabla ya mabadiliko, wananchi walitakiwa kufuatilia hati kwenye ofisi za kanda ambazo zipo mbali, jambo ambalo lilichelewesha upatikanaji wa nyaraka hiyo muhimu kwa umiliki wa ardhi.

Kutokana na hali hiyo idadi ya wananchi waliomudu gharama za kufuatilia hati ni chache, na wale zilizobakia walipata matatizo mbalimbali na kujicheleweshea maendeleo.

Urasimu katika sekta ya ardhi ulisababisha urasimishaji wa ardhi kuchelewa hadi pale serikali ilipoamua kurahisisha na sasa kumekuwa na hati za makazi zilizowezesha kuongeza thamani ya ardhi.

Sekta hiyo huko nyuma ilitawaliwa na rushwa kiasi cha mwenye nguvu ya fedha alifanya awezalo kupora haki ya maskini, huku kukiwa na ushiriki mkubwa wa watumishi wa idara hiyo, jambo ambalo liliwaweka wananchi katika maumivu na mahangaiko makubwa.

Waziri huyo ameeleza bayana kuwa utaratibu wa sasa hati za maeneo husika zinapokamilika halmashauri husika izifuate kwa Msajili wa Hati azifuate katika ofisi ya ardhi mkoa badala ya wananchi kuzifuata mkoani.

Tunapongeza hatua hii kwa kuwa sasa inakwenda kutoa ahueni kubwa kwa wananchi ambao licha ya kupitia misukosuko kwa ajili ya kupata hati miliki, lakini bado walilazimishwa kusafiri mbali na kutumia fedha kupata hati husika.

Pia, kupatikana kwa hati na leseni za makazi kumeongeza thamani ya ardhi na sasa mmiliki anaweza kupeleka hati yake kwenye taasisi ya fedha na kupata mkopo utakaomwezesha kuwekeza kwa ajili ya maendeleo ya sasa na yajayo.

Kipindi cha nyuma, wananchi wengi hususan maskini hawakukopesheka kwa kuwa hawakuwa na hati ya kuweka kama dhamana ili waaminiwe, lakini kwa sasa kupitia hati na leseni hizo wanakopesheka, na itapunguza au kumaliza migogoro ya ardhi.

Hii ni hatua kubwa na ambayo imeiwezesha serikali kupata mapato kutokana na makazi ambayo zamani haikukusanywa kwa kuwa maeneo husika yalikuwa hayajapimwa na kupewa hati au leseni.

Baada ya kauli ya Waziri, kinachotarajiwa ni utekelezaji kwa kuhakikisha mwananchi anapata hati kwenye halmashauri na kusiwe na ubabaishaji wowote au kujenga mazingira ya ugumu ili mwananchi atoe rushwa.

Kwa wakati huu, wananchi wanapaswa kuitumia vyema fursa hii kwa kuhakikisha kila mtu anafuatilia na kuchukua hati yake, hivyo kufikia malengo husika.

Tunaipongeza wizara, lakini ufuatiliaji ni muhimu sana kuhakikisha hati zinapatikana katika ngazi hiyo na kwa wakati mwafaka, kwa kuwa kuongea au kuagiza huwa ni jambo moja, lakini utekelezaji ni jambo jingine ambalo huhitaji msukumo mkubwa.

Lakini pia, taasisi za fedha zinapaswa kupokea hati hizo na kujiridhisha nazo kisha kutoa huduma ya mikopo kwa mujibu wa taratibu zao, hivyo kuwawezesha kusonga mbele kimaisha kwa kuwa watawekeza kibiashara, makazi na mengineyo.

Kutokana na hatua hii, sasa tunaweza kusema kuwa serikali inaonyesha kwa vitendo ahadi zake za kuwajali wanyonge kwa kuhakikisha wanapata huduma muhimu, ambazo humo nyuma ilikuwa ndoto kuzipata, hususan hati ardhi.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



# Ni zamu ya wapigakura kuwachuja wagombea

Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya wanasiasa kutoka vyama mbalimbali vya siasa, wameshatangaza nia ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Hatua hiyo inatokana na baadhi ya vyama hivyo kuwataka wanachama wake wenye nia ya kutaka uongozi, kujitokeza ili kupimwa kama wanatosha kuviwakilisha kwenye uchaguzi huo.

Pamoja na milango ya baadhi ya vyama kufunguliwa, siyo vibaya wapigakura kujipa nafasi ya kuwachunguza na kuwapima watiania hao kama wanatosha, kwa lengo la kupata viongozi bora wa kuwaongoza.

Iwapo hawatafanya mchakato huo 'wasiotosha' hivyo kubaki kulalamika.

Ikumbukwe kwamba kila unapofanyika uchaguzi, watu wengi wanajitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, wakiwamo hata wale wasio na sifa ili mradi tu wapae uongozi.

Hivyo suala la kuwachunguza ni la muhimu kama ambavyo, Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA) inavyosisitiza, lengo likiwa ni kupata viongozi bora na siyo bora viongozi.

Binafsi ninaunga mkono ushauri huo wa CEGODETA, ambao unalenga kusaidia Tanzania kupata viongozi wanaofaa na wanaowatumikia wananchi.

Ni kweli, wanachama wa vyama mbalimbali vya siasa na wasio na vyama, wanawajua watu ambao wanafaa kuwaongoza na wakati mwingine ni wale wanaoishi nao, hivyo njia nzuri ni kuanza kuwachunguza.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Thomas Ngawaiya, inatamani wapigakura wasijigawe kwa itikadi za vyama vya siasa na badala yake kumpendekeza yule wanayeamini anaweza kuwaongoza.

Jambo la kuzingatia liwe kutambua umuhimu wa watu wanaofaa kuongoza bila kujali mambo ya vyama, kwa vile maendeleo hayana chama ili mradi wanayemtaka ana uwezo wa kuongoza.

Anatambua kuwa ni lazima watia nia wapitie kwenye mchakato wa kura za maoni, katika vyama vyao, lakini wapigakura wana nafasi ya kuchunguza na kushawishi au kushauri ili kupata mgombea sahihi.

Kimsingi, ushauri huu ukizingatiwa, unaweza kusaidia kuleta maendeleo kwenye ngazi mbalimbali ikiwamo kata na majimbo, lakini ni vyema kuwe na angalizo katika jambo hili.

Angalizo ni kwamba ni muhimu kuzingatia jinsia kwenye uongozi, kwani katika jamii, bado kuna watu ambao wanawatenga wanawake wakiamini kuwa hawana uwezo wa kuongoza.

Dhana hiyo imeshapitwa na wakati, ni vyema sasa jamii ikabadilika na kutambua kuwa wanawake nao wana uwezo wa kuongoza kama walivyo wanaume, na inawezekana wapo wanaowazidi wanaume.

Kwa maana hiyo, mtiania awe mwanamke au mwanaume, wote wana haki ya kuchaguliwa na kuchagua, ili mradi wapigakura wamemchunguza na kuona mmoja wao anafaa, basi awe chaguo lao.

Suala la ubaguzi wa kijinsia lisipewe nafasi, kwa sababu linasababisha watu wenye sifa za kuongoza kukosa nafasi kutokana na jamii kuendekeza mila na desturi ambazo zimepitwa na wakati.

Uongozi ni wito, hivyo mtu akiwa kiongozi ni lazima ajijengee mazingira mazuri ya kuwa mfano wa kuigwa na watu wengine ili hata anapohitaji kuchaguliwa kwa mara nyingine, iwe rahisi kupata kura.

Ninaamini kwamba kwenye jamii, watu hao wapo wakiwamo wanaume na wanawake, na pia wapo pia wale, ambao hawajawahi kuongoza, lakini wameonyesha kuwa wakipewa nafasi wanaweza kuongoza.

Watu wa aina hii kama anavyosema Ngawaiya, wasiachwe, bali wapigakura wawafikirie pia, hivyo ikiwa imebaki miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu, ni vyema wapigakura nao wakajiwekea mbinu za kupata watu wanaofaa.

Wakati huu ambao michakato mbalimbali ikiendelea kufanyika kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi huo, wapigakura nao hawana budi kuwa na mchakato wao wa kimya kimya.

Uandikishaji wa watu, katika daftari la kudumu la wapigakura, utoaji wa elimu ya mpigakura ni miongoni mwa mambo ya muhimu katika uchaguzi huo, lakini wapigakura nao wawe wabunifu katika hili.

Kwa mujibu wa Ngawaiya katika siasa kuna mambo mengi yanafanyika ikiwamo watu wasio na sifa za kuongoza lakini nao hujitokeza kuwania uongozi.

# TIGO yazindua huduma mpya iliyoboreshwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano ya TIGO Tanzania, imezindua huduma mpya iliyoboreshwa inayomwezesha mteja wake kununua muda wa maongezi pamoja na vifurushi kutoka katika maduka yake.

Aidha, huduma hiyo inapatikana katika maduka ya rejareja yanayotambuliwa na TIGO Tanzania.

"Huduma hii ya TIGO Rusha iliyoboreshwa itatolewa katika mtandao wa mauzo wa TIGO pamoja na maduka ya TIGO, mawakala wa TIGO Pesa, wauzaji wa kujitegemea, pamoja na katika vituo vya mauzo nchi nzima. Pamoja na huduma nyingine zilizopo, huduma hii itaongeza wigo wa namna ya kuongeza salio kwa wateja," alisema Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa TIGO Tanzania, David Umoh.

Umoh alisema: "Tumejizatiti kuimarisha na kubuni njia zenye kuleta unafuu na zenye chaguzi nyingi ili kumpatia mteja fursa ya kuchagua huduma inayoendana na mahitaji yake kulingana na sehemu aliyopo na muda husika. Tunafanya maboresho haya ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia na maisha kwa ujumla."

"Wateja wetu wakae mkao wa kula kwamba sasa wataweza kununua muda wa maongezi pamoja na vifurushi kutoka kwenye maduka yetu pamoja na wauzaji wengine wanaotambuliwa na TIGO nchi nzima.

"Tigo Rusha haina changamoto za kuharibika kwa karatasi ya vocha za kukwangua, lakini huduma hii inampunguzia adha mteja wetu wa kutembea na kadi za vocha pindi anapohitaji kuongeza salio kwenye simu yake."

Aliongeza: "Tigo Rusha inawapa wateja wake thamani ya pesa zao kwa maana huduma hii ni rahisi sana kutumia, salama na ya uhakika. Kila mteja wa TIGO atakeyenunua salio au kifurushi chochote kupitia huduma hii ya Tigo Rusha anapewa zawadi ya nyongeza."

Umoh pia aligusia manufaa watakayopata wauzaji pamoja na mawakala watakapofanya mauzo yao kwa kutumia njia hii mpya ya TIGO Rusha iliyoboreshwa.

Kadhalika, alieleza matokeo ya matumizi ya huduma hiyo kwa maelfu ya wasambazaji wa vocha za kukwangua nchi kote.

"Napenda kuwahakikishia wasambazaji wetu wote wa vocha za kukwangua kwamba hii ni fursa mpya ya kuongeza kipato, hivyo ni fursa pia kwao kukua pamoja na TIGO na kama kampuni tutaendelea kuwaunga mkono wasambazaji wote wa vocha hizo za kukwangua kote Tanzania," alisema Umoh.



Mjumbe wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Henry Mwimbe, akikagua transifoma zilizopo kwa ajili ya kusambazwa kwenye vijiji vya eneo la mradi wa usambazaji nishati ya umeme unaotekelezwa na Kampuni ya CCCE Co Ltd, mradi huo ulikaguliwa katika vijiji vya Wembere na Ntwike Wilaya ya Iramba, mkoani Singida jana. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# RC aagiza watumishi 34 wakamatwe

**Na Allawi Kaboyo,** BIHARAMULO

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ameagiza kukamatwa kwa watumishi 34 wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, wakiwamo watendaji wa vijiji na kata kwa kushindwa kurejesha Sh. milioni 307 zilizokusanywa kutoka vyanzo vya mapato ya ndani bila kupelekwa benki.

Alitoa hilo jana kwa Kamanda wa Polisi mkoani humo na Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kagera, alipozuru wilayani humo kutoa maelekezo ya kiutendaji kutokana na halmashauri hiyo kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato, huku kikibainika ubadhirifu wa fedha za serikali.

Aliagiza kukamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi watumishi hao, mamlaka kuwasimamisha kazi Kaimu Mwekahazina, Sospiter Makene, maofisa wa TEHAMA, Jastine Banula na Rogers Semukoko pamoja na Ofisa Biashara, Beatrice Gurusya, wote watumishi wa halmashauri hiyo.

Gaguti amechukua uamuzi huo baada ya kutoa siku saba kwa watumishi hao kurejesha fedha hizo alipozungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichofanyika Juni 5 mwaka huu kwa lengo la kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

"Nilikuja hapa nikatoa maelekezo kwa wale wote waliokuwa wanakusanya fedha kwa kutumia mashine za Poss bila kuzipeleka benki kuwa warejeshe fedha na nikawapa siku saba, lakini fedha iliyorejeshwa ni asilimia mbili.

"Kwa mwendo huu, hatuwezi kwenda, lazima tuweke misingi imara ya kuboresha utumishi na uadilifu, hapa nina orodha ya watendaji 30 ambayo nampati Kamanda wa Polisi kuhakikisha watu hao wanakamatwa popote walipo na wengine wanne hawa ninaagiza wasimamishwe kazi, lakini wawe chini ya uangalizi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, ili kutoa ushirikiano," aliagiza.

Alisema watumishi wa umma wanatakiwa kuwa waadilifu na kuiogopa fedha ya serikali na kuahidi kuwachukulia hatua wote watakaobainika kufanya vitendo vya ubadhirifu.

Pia, aliwataka watendaji wa vijiji na kata mkoani humo kuhakikisha wanasimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali bila kuleta 'ujanjaujanja'. "Fedha ya serikali ni ya moto, hivyo haipaswi kulala, niwasihi tu ndugu zangu tusijaribiane, hatutasita kumchukulia hatua yeyote atakayehusika na upotevu wa pesa.

"Tambueni watendaji ndiyo mna dhamana ya kukusanya mapato ya ndani kutoka katika vyanzo vya mapato katika maeneo yenu," aliagiza.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema kuna baadhi ya watumishi walikataa kusajili vyanzo vya mapato kwa makusudi na baadaye kurudi kwa wafanyabiashara na kuchukua fedha kinyemela na kusababisha serikali kukosa mapato yake.

# Idris Sultan anusurika kufutiwa dhamana

**Na Hellen Mwango**

MCHEKESHAJI Idris Sultan (27), jana alinusurika kufutiwa dhamana baada ya kuchelewa kufika mahakamani kusikiliza kesi inayomkabili na wenzake wawili ya kurusha maudhui mtandaoni bila kuwa na leseni.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, ilianza shughuli zake saa 3:00 asubuhi.

Kesi ya Idris iliitwa, wenzake wawili walipanda kizimbani, lakini msanii huyo hakuwapo mahakamani wala wadhamini wake.

Wakili wa Serikali, Esther Martin, alidai kutokuwa na taarifa za mshtakiwa huyo.

Hakimu Shaidi alisema mahakama yake inatoa hati ya kukamatwa Idrisa ili afike kujieleza kwanini hakufika mahakamani. Hata hivyo, saa 4:05 asubuhi, mshtakiwa alifika mahakamani.

Idris alijitetea kwamba alichelewa kutokana na hitilafu za kiafya.

"Mheshimiwa nimechelewa kwa sababu tumbo langu lilipata hitilafu, ninaomba unisamehe," Idris alidai.

Hakimu alisema anafahamu hakuwa na shida ya tumbo na kwamba kama tatizo ni usafiri upo usafiri wa serikali.

"Kama tatizo usafiri usiwe na wasiwasi upo usafiri wa serikali wa kukuleta mahakamani kwa wakati na kukurudisha bure bila gharama, mahakama hii inatengua hati ya kukamatwa kwako, kesi itatajwa Julai 28 mwaka huu," Hakimu Shaidi alisema.

Mbali na Idrisa, washtakiwa wengine ni Doctor Ulimwengu (28) na Isihaka Mwinyimvua (22).

Awali, Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Baltilda Mushi, ulidai washtakiwa hao walitenda kosa hilo kati ya Machi 8 mwaka 2016 na Machi 12 mwaka huu katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.

Baltilda alidai washtakiwa hao walirusha maudhui kupitia televisheni ya mtandaoni kwenye akaunti ijulikanayo Loko Motion bila kuwa na leseni kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA).

Washtakiwa walikana mashtaka na upande wa mashtaka ulidai upelelezi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

# Majaliwa: Umeme utafikishwa kila kijiji

**Na Mwandishi Wetu,** Ruangwa

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ya awamu ya tano imedhamiria kufikisha huduma ya umeme katika vijiji vyote nchini vikiwamo 25 vya Wilaya ya Ruangwa ambavyo bado havijafikiwa na umeme.

Kufuatia hatua hiyo, Waziri Mkuu amewataka wananchi walio katika vijiji ambavyo bado havijaunganishiwa nishati ya umeme wafanye maandalizi kwa sababu maeneo mengine tayari makandarasi wameshapatikana.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi katika vijiji vya Nanjaru, Nambilanje, Mkaranga, Namichiga na Mbekenyera akiwa kwenye ziara yake ya kikazi Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi.

Alisema Wilaya ya Ruangwa ina jumla ya vijiji 90 kati yake vijiji 25 tu ndio bado havijafikiwa na huduma ya umeme, lakini tayari mkandarasi ameshapatikana na ameshaanza kazi, hivyo aliwataka wananchi wajiandae kuunganisha umeme kwenye nyumba zao za makazi na biashara.

"Rais wetu Mheshimiwa Dk. John Magufuli anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inawaka umeme na amepunguza gharama za kuunganisha umeme kutoka Sh. 380,000 hadi Sh. 27,000 ili kila mwananchi aweze kumudu gharama hizo."

Waziri Mkuu aliongeza kuwa licha ya gharama za kuunganishiwa umeme kupunguzwa, pia wananchi hatolazimika kulipia gharama za nguzo pamoja na gharama za fomu za maombi ya kuunganishiwa umeme kwani tayari zimeshalipiwa na serikali.

Vilevile, Waziri Mkuu alisema serikali imeboresha huduma za afya kwa kuhakikisha kuwa dawa na vifaa tiba vinapatikana katika maeneo yote ya kutolea huduma za afya na kwamba haitaki kuona mwananchi anakwenda maeneo hayo na kukosa huduma.

"Mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli alipoingia madarakani aliongeza bajeti ya dawa kutoka Sh. bilioni 31 na kufikia Sh. bilioni 269, hatutarajii kusikia mgonjwa amekwenda zahanati akaandikiwa cheti na kisha akaelekezwa kwenda kununua dawa kwenye maduka ya watu binafsi."

Waziri Mkuu amesema ni lazima dawa zipatikane katika maeneo yote ya kutolea huduma za afya kulingana na hadhi ya eneo husika kama zahanati lazima dawa zinazotakiwa kuwapo kwenye zahanati ziwepo, kadhalika kituo cha afya na hospitali.




Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, akizungumza na waandishi wa habari jijini Tanga jana, baada ya kikao cha wadau wa Kamati ya Amani ya mkoa wa Tanga. Kulia ni Mkuu wa mkoa huo, Martin Shigella. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Malipo ya pamba kutopitia AMCOS

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

KATIKA kupambana na upotevu wa fedha za wakulima wa pamba, Halmashauri za Mbogwe na Bukombe mkoani Geita, serikali imeanzisha utaratibu wa kuwalipa wakulima fedha za mauzo ya zao hilo kupitia taasisi za kifedha badala ya kupitia kwenye vyama vya msingi (AMCOS) ilivyokuwa awali.

Benedicto Bulugu, Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mbogwe-Masumbwe (MBCU), aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari kuhusiana na alivyojipanga kutatua kero ya wakulima wa pamba ambao kila msimu fedha zao zimekuwa zikichelewa kuwafikia.

Alisema katika msimu uliopita wa 2018/19, wakulima wengi walidhulumiwa fedha zao na baadhi ya viongozi wa vyama vya msingi kwa kuwahadaa kuwa hawajalipwa na kampuni za ununuzi wa zao hilo, huku fedha hizo zikitumika kusafirishia pamba.

Bulugu alisema mwaka jana zaidi ya shilingi milioni 100 fedha za wakulima ziliibwa na baadhi ya viongozi wasiokuwa waaminifu na kusababisha serikali kuingilia kati kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwakamata viongozi hao ambao baadhi yao walizirudisha.

"Kampuni zinanunua pamba na kulipa fedha kwenye vyama vyetu vya msingi, viongozi wanashindwa kuwalipa wakulima wetu fedha zao kwa kisingizio kuwa hawajalipwa na kampuni husika...ukifuatilia fedha zimeshalipwa na viongozi wanazifanyia kazi ya kununua pamba upya," alisema Bulugu.

Aliongeza: "Mwaka huu mkulima atalipwa fedha zake kupitia akaunti yake ya benki, na wameshafungua katika benki za NMB na CRDB, tutahakikisha yaliyojitokeza msimu uliopita hayajirudii tena ili kuhakikisha wakulima wetu wananufaika na kilimo chao."

Makamu Mwenyekiti wa MBCU, Salum Kayumbo, alisema msimu huu wanatarajia kuvuna kilo milioni 10 za pamba na zitachakatwa katika kiwanda chao, ambacho kimeshaanza kufanya na kuwataka wakulima kutunza pamba katika hali ya usafi.

Naye Yona Kisena, mkulima wa pamba wa Chama cha Msingi Mwanza MADASO, aliipongeza serikali kwa kuleta mfumo wa malipo kupitia taasisi za kifedha, na kuwa utakaopunguza malalamiko yao dhidi ya viongozi wa AMCOS.

# FORUMCC yataka uwekezaji zaidi katika nishati jadidifu

**Na Halfani Chusi**

SHIRIKA Lisilo la Kiserikali Linalojihusisha na Kuleta Ushawishi wa Kuchukua Hatua za Kustahimili Athari za Mabadiliko ya Tabia ya Nchi (FORUMCC), limeshauri serikali kutoa kipaumbele katika sekta binafsi kufanya uwekezaji kwenye nishati jadilifu.

Vilevile, limeishauri serikali kuongeza nguvu zaidi katika kuvutia uwekezaji wa viwanda vinavyotumia malighafi ya mazao na mimea.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa shirika hilo, Rebecca Muna, alipozungumza na waandishi wa habari, akipongeza juhudi za serikali katika kuanzisha ujenzi wa mtambo wa kuzalisha nishati itokanayo na jotoardhi katika Mto Ngozi jijini Mbeya na kubuni nguvu itakayobuni nguvu ya umeme utokanao na upepo wilayani Mfundi, Iringa.

"Tanzania tumebarikiwa vyanzo vingi vya nishati kama jua, jotoardhi, maji, upepo na mabaki ya mazao (biomass), ambavyo ni mbadala wa nishati ya mafuta, makaa ya mawe na gesi asilia. Tukivitumia vizuri, tunaweza kuzalisha nishati ya kutosha na kukidhi mahitaji ya nchi kwa ujumla kwa gharama nafuu," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisema kuwa uwekezaji wa nishati jadilifu utaongeza upatikanaji wa ajira nchini.

"Kupitia nishati jadilifu, wanawake pia watapata ahueni ya kutafuta nishati ya kuhudumia familia na kufanya biashara ndogondogo. Pia vijana watahusishwa kutumia fursa shirikishi zitakazotokana na nishati jadilifu, itasaidia kuongeza ajira katika sekta ya kilimo na biashara," alibainisha.

Mratibu Mradi wa FORUMCC, Henry Kazula, aliishauri serikali kuachana na kaulimbiu ya 'Kata Mti Panda Mti' na badala yake ibuni mbinu mbadala kama nishati jadilifu itakayosaidia kuepusha ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa.

"Ukikata mti leo na ukapanda mti mwingine leo, kwa mti mwingine hadi kuja kufikia hatua ya kukata tena ni zaidi ya miaka 10. Takwimu zinaeleza zaidi ya ekari 300,000 zinateketea kutokana na mahitaji ya mkaa.

"Sasa, ni vyema serikali ingeendelea kutoa kipaumbele kwa sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya nishati jadilifu ambayo itasaidia uzalishaji wa nishati ya kutosha na kusaidia watu kuachana na matumizi ya mkaa na kutumia zao la nishati jadilifu," alishauri.

# ‘Watoto wapewe elimu kuhusu rushwa ya ngono’

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI wa Asasi Isiyo ya Kiserikali inayojihusisha na Masuala ya Utetezi wa Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, ameishauri jamii kuanzisha klabu zitakazojihusisha na utoaji wa elimu kwa watoto kutambua haki zao.

Mawinza alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salam katika kumbukizi ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo ilifanyika Juni 16, akisisitiza umuhimu wa klabu kutoa elimu kwa watoto, hususani katika kutambua haki zao, elimu juu ya rushwa ya ngono pamoja na namna ya watoto wanavyoweza kupigania na kujua haki zao ambazo kimsingi zitawasaidia kutimiza ndoto zao.

“Sisi kwa sasa tumeshaanzisha klabu ya utoaji wa elimu kwa watoto juu ya kutambua haki zao za msingi pamoja na namna ya wao kujikinga na masuala ya unyanyapaa, ambapo kwa sasa tuna wanafunzi kutoka shule za sekondari na msingi pamoja na watoto ambao wapo mitaani.

“Tunaendelea kuwapa elimu, hadi sasa watoto wengi wamepata elimu na wameanza kutambua haki zao za msingi,” Mawinza alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa watoto wengi wamekuwa wakishindwa kufikia malengo yao kwa kukosa elimu juu ya masuala ya rushwa ya ngono, ambayo mambo hayo kimsingi yamekuwa yakikatisha masomo ya wanafunzi, na wengine kuharibiwa kabisa kiafya.

Mmoja kati ya wanafunzi hao ambao wamekuwa wakipata elimu hiyo kutoka Shule ya Msingi Makumbusho, Happy Boniventure, alisema wamepata uelewa mkubwa kutokana na elimu wanayoopata na kwamba kwa sasa wanatambua haki zao za msingi na namna ya kujiepusha na vitendo vinavyoashiria rushwa ya ngono.

“Tunawashukuru Women Fund kwa kufadhili huu mradi pamoja na mkurugenzi wetu Janeti Mawinza, kwa kuwa kwa sasa tumepata elimu kubwa sana na mambo mengi tulikuwa hatuyajui, lakini sasa tumeyajua,” alisifu.

Mwalimu Mlezi anayeongoza klabu hiyo, Monika Alex, alisema licha ya kuendelea kutoa elimu, bado wanakabiliana na tatizo la wazazi kutowaruhusu watoto kuhudhuria mafunzo.

# Hati za ardhi kutolewa ndani ya wiki moja

**Na Munir Shemweta,** TANGA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeeo ya Makazi, William Lukuvi, ameagiza kutolewa hati za umiliki wa ardhi ndani ya wiki pamoja pale mwananchi atakapokuwa amekamilisha taratibu zote za umilikishwaji ardhi.

Aidha, ameagiza wananchi kupatiwa hati zao za ardhi katika halmashauri waliolipia gharama za kupatiwa hati ili kuondoa usumbufu pamoja na gharama kwa mwananchi kufuatilia hati kwenye ofisi za ardhi za mikoa.

Lukuvi alitoa agizo hilo jana wakati akizindua ofisi ya ardhi mkoa wa Tanga katika hafla fupi iliyofanyika jijini Tanga. Uzinduzi wa ofisi hizo ulihudhuriwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu; Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo; Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela; Kamishna wa Ardhi nchini, Nathaniel Nghode; Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Judica Omari; wakuu wa wilaya za mkoa wa Tanga pamoja na viongozi wa taasisi mbalimbali za mkoa huo.

Lukuvi alisema wizara yake imekamilisha ndoto za Rais John Magufuli za kuondoa usumbufu kwa wananchi kupata hati za ardhi pamoja kufuata huduma za ardhi umbali mrefu na kutolea mfano kuwa, mkazi wa mkoa wa Tanga alilazimika kuifuata huduma ya ardhi mkoani Kilimanjaro.

“Umekamilisha taratibu zote za kupatiwa hati hapa Tanga, unaambiwa ukachukue Moshi ilipo ofisi ya Kanda, Rais ameliona hilo maana gharama za ufuatiliaji ni kubwa kuliko hata gharama ya kulipia hati yenyewe” alisema Lukuvi.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuhakikisha pale hati za maeneo yao zinapokamilika wamfuate msajili msaidizi wa hati katika ofisi ya ardhi ya mkoa kwa lengo la msajili huyo wa hati kwenda kuzikabidhi hati hizo kwa wahusika kwenye halmashauri badala ya wananchi kuziafuta mkoani.

Kwa mujibu wa Lukuvi, kumbukumbu zote za ardhi katika mkoa zilizokuwa ofisi za kanda nazo zimepelekwa mikoa husika na kutolea mfano kumbukumbu za mkoa wa Tanga ambazo awali zilikuwa zikihifadhiwa Dar es Salaam na baadaye kuhamishiwa Moshi, Kilimanjaro sasa zimetunzwa ofisi ya ardhi mkoa wa Tanga.

Alizitaja baadhi ya kumbukumbu zilizo katika Ofisi ya Ardhi mkoa wa Tanga kuwa, ni michoro zaidi ya 1,026, ramani 5,400 pamoja na hati 18,460 na kusisistiza kuwa hati pamoja na nyaraka nyingine zimetunzwa vizuri na wamiliki wake wanaweza kukopesheka bila matatizo

Waziri Lukuvi aliongeza kuwa tangu kufunguliwa kwa ofisi mpya ya ardhi mkoa wa Tanga, hati zaidi ya 300 zimeandikwa na kusajiliwa kwenye mkoa na kusisitiza kuwa, uanzishwaji ofisi za ardhi kwenye mikoa siyo tu utaondoa usumbufu wa kufuatilia hati bali utapunguza pia migogoro ya ardhi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, alisema jitihada zilizofanywa na serikali kuanzisha ofisi za ardhi za mikoa zina lengo la kumpunguzia mwananchi usumbufu wa kufuata huduma ya sekta hiyo umbali mrefu, ambapo huduma hiyo ilikuwa ikipatikana ofisi za kanda na kila kanda ilikuwa ikihudumia mikoa mitatu au zaidi.

Alisema, serikali kupitia wizara yake inakusudia ardhi yote nchini ipangwe, kupimwa na kumilikishwa ili wananchi waweze kupewa miliki, huku hatua hiyo ikilenga pia kupunguza migogoro ya ardhi nchini.




Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utalawa wa Benki ya TPB, Diana Myonga (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa mabati 100 kwa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Singida, Ayshrose Matembo (wa nne kulia), kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa shule za sekondari na msingi mkoani Singida. Wengine ni wananchi mbalimbali na wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji Kiongozi ahimiza huduma bora mahakama

**Na Lydia Churi,** MAHAKAMA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Dk. Eliezer Feleshi, amesema uzuri wa majengo ya mahakama yanayojengwa hivi sasa haunabudi kuambatana na upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

Akizindua jengo jipya la Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Simiyu pamoja na Mahakama ya Wilaya ya Bariadi, Jaji Kiongozi pia amewataka watumishi wa mahakama nchini kubadili mienendo na tabia zinazokiuka miiko na maadili ya kazi na utumishi wa umma ili waweze kutoa huduma kwa ubora unaostahili.

“Natoa rai kwa viongozi wote kuhakikisha kwamba watumishi wote wa mahakama wanatoa huduma nzuri zinazoendana na uzuri wa majengo, tujiepushe na lugha zisizofaa kwa wateja wetu ambao ni wananchi na wadau, tujiepushe na vitendo vya rushwa kwani rushwa ni adui wa haki,” alisema.

Alisema mahakama haitasita kumchukulia hatua kali za kinidhamu na kisheria mtumishi yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya rushwa. Aliwaomba wakuu wa mikoa na wilaya kupitia Kamati za Maadili ya Mahakimu kuwaelimisha wananchi kutumia kamati hizi kuwasilisha malalamiko ya mienendo isiyofaa kwa baadhi ya mahakimu wanaokiuka maadili wanapotekeleza majukumu yao ya msingi ya utoaji haki.

Jaji kiongozi alisema uwapo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Simiyu ni nafuu na ukombozi kwa wananchi wa Simiyu, kwani awali walikuwa wakisafiri umbali wa kilometa 140 kwenda mkoani Shinyanga kufuata huduma za mahakama. Alisema umbali huo mrefu uliwaathiri kwa kutumia muda wao mwingi kutafuta haki na pia wengine waliikosa haki kwa kukata tamaa na kushindwa kumudu gharama za kujikimu kwenda mkoani Shinyanga.

# Bil.12/- kukipanua Chuo cha Diplomasia

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Diplomasia na Uhusiano wa Kimataifa (CFR) cha jijini Dar es Salaam, kinarajia kutumia kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 12 za Kitanzania kwa ajili ya kujipanua, ikiwamo ujenzi wa majengo mapya na kuanzisha kampasi mpya mikoani.

Lengo ni kuongeza idadi ya wanufaika wa programu na kozi zinazotolewa na chuo hicho. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mkurugenzi wa Chuo hicho, Dk. Jeremia Ponera, alisema kujipanua kwa chuo kunakwenda sambamba na kuongeza programu na kozi mbalimbali ili kukidhi mahitaji na mahitaji ya soko la ajira nchini.

"Tunapenda kuishukuru Serikali ya Rais Dk. John Magufuli kwa kutenga fedha kwa ajili ya upanuzi wa chuo hiki. Tutajenga vyumba vya mihadhara, maabara ya lugha, maktaba ya kisasa, vyumba vidogo vya kufundishia na semina, hosteli za wanafunzi pamoja na maeneo ya kujifunzia," alisema Dk. Ponera.

Dk. Ponera alisema mradi wa upanuzi wa chuo utasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 1,500 hadi kufikia 4,000 kwa Dar es Salaam peke yake.

"Tunatarajia kufungua kampasi tatu Dodoma, Arusha na Zanzibar ili kupanua wigo na kutoa fursa kwa Watanzania wengi wenye kiu ya kujiunga na programu pamoja na kozi mbalimbali waweze kufikiwa kwa haraka," alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo elimu inayotolewa na CFR itakuwa imewafikia Watanzania wengi mikoani ambao walikuwa wanalazimika kuja Dar es Salaam kwa ajili ya kujiunga na programu na kozi mbalimbali zinazotolewa na chuo.

"Tumeshafika Dodoma na tupo katika hatua za mwisho za kupata ardhi na kuanza ujenzi na tunategemea katika kipindi cha miaka mitatu ijayo tutakuwa tumekamilisha ujenzi wa kampasi yako," alisema Dk. Ponera na kuongeza kuwa chuo kimeshapata pia kiwanja katika mkoa wa Arusha.

Alisema CFR kimejipanga kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025, sambamba na kujenga ufahamu, kuvutia uwekezaji na biashara za kimataifa.

# Kairuki avutiwa uwekezaji mkubwa kongani ya Ihemi

**Na Mwandishi Wetu, I**RINGA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki, amepongeza uwekezaji mkubwa uliofanyika katika Kongani ya Ihemi kwenye ushoroba wa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) na kuwataka wakuu wa mikoa katika eneo hilo kushirikiana na wawekezaji kwa karibu kutatua changamoto ili kuongeza uzalishaji.

Akizungumza kwa nyakati tofauti alipotembelea kiwanda cha kuzalisha maziwa cha ASAS Dairies Farm Limited, GBRI Solutions Tanzania Ltd na Farm for the Future, Kairuki alisema uwekezaji katika eneo hilo umekuwa na mchango mkubwa kwa kuongeza mnyororo wa thamani za mazao pamoja na kuinua sekta ya maziwa.

"Wakuu wa mikoa katika ushoroba wa SAGCOT ni vizuri wakashirikiana pia na kituo cha uwekezaji nchini kwani uwekezaji huo umeshatoa matokeo chanya kwa kubadilisha maisha ya watu na kuongeza kipato cha taifa," alisema Kairuki ambaye yupo katika ziara ya kutembelea mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya ili kukagua na kujionea shughuli za uwekezaji pamoja na kuzungumza na wawekezaji katika mikoa hiyo.

Katika ziara hiyo waziri aliipongeza SAGCOT pamoja na Ofisa Mtendaji wake Mkuu, Geoffrey Kirenga, kwa kuwa mfano mzuri katika kuhamasisha uwekezaji kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), na kuzitaka taasisi zingine kuiga mfano huo.

"Siyo jambo la kuficha kwani maeneo ya uwekezaji katika mikoa ya Iringa Mbeya na Njombe ni makubwa na mazuri kwa shughuli za kilimo na ufugaji, hivyo wakati umefika kwa wawekezaji kuendelea kuchangamkia fursa zinazojitokeza kwa kujisajili TIC na kunufaika na fursa za vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi," alisema.

Kairuki alisema wakati umefika kuangalia miradi katika eneo zima la kongani ya Ihemi ambayo bado haijasajiliwa TIC, ikasajiliwe ili mwekezaji aweze kunufaika na fursa za vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi zinazotolewa kwa mwanachama pekee.

Alisema serikali ya awamu ya tano inatambua mchango wa uwekezaji wenu na ndiyo maana inaboresha miundombinu muhimu ikiwamo uwepo wa nishati ya umeme ya uhakika, barabara bora, upatikanaji wa majisafi, kuboresha mifumo ya mawasiliano na upatikanaji wa huduma bora za mamlaka zinazosimamia masuala yanayohusu uwekezaji nchini.

Naye Mkurugenzi wa kiwanda cha maziwa cha ASAS, Fuad Abri, aliipongeza serikali kwa hatua madhubuti wanazozichukua kuhakikisha wanaboresha mazingira ya uwekezaji ikiwamo miundombinu sambamba na kuanzisha dawati la sekta binafsi katika sekta ya ufugaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha GBRI Solution Tanzania Ltd kinachojihusisha na usindikaji wa matunda na mboga, Hadija Jabiri, alisema mbali ya mafanikio anayoyapata amekuwa akikumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo kushindwa kukidhi mahitaji ya soko la nje kwa kushindwa kufikisha mzigo sokoni kwa muda uliopangwa.

Naye Kirenga alisema kituo kitaendelea kuunganisha nguvu kutoka sekta za umma na binafsi ili kutoa mchango stahiki wa maendeleo na ukuaji wa sekta ya kilimo na mifugo nchini.




Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, Emmanuel Makala (kulia), akikabidhi vifaa vya kisasa vya kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kwa wakuu wa majimbo na wachungaji wa kanisa hilo, mikoa ya Shinyanga na Simiyu kwa ajili ya kuendeleza mapambano dhidi ya virusi vya corona, kushoto ni Mchungaji Patrick Zengo wa Usharika wa Kaanani Ndembezi Manispaa ya Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**.

# Askofu aasa wananchi kuhusu corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi Kusini Masharika ya Ziwa Victoria mikoa ya Shinyanga na Simiyu, Emmanuel Makala, amewataka wananchi kutovidharau virusi vya corona, bali waendelee kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi.

Alibainisha hayo jana wakati akikabidhi vifaa vya kisasa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, kwa wakuu wa majimbo pamoja na wachungaji wa kanisa hilo kutoka mikoa ya Shinyanga na Simiyu, kwa ajili ya kuendeleza mapambano ya kuzuia maamhukizi ya ugonjwa huo kwa kushirikiana na Kanisa la Kiinjili Kiluther Bavaria la Ujerumani.

Alisema licha ya maambukizi ya virusi vya corona kupungua nchini, ni vyema wananchi wasividharau virusi hivyo, bali waendelee kuchukua tahadhari ya kujikinga pamoja na kufuata maelekezo ya serikali ili waendelee kuwa salama, kwa kunawa mikono, kuvaa barakoa, kupaka vitakasa mikono, na kutokaa katika mikusanyiko.

"Natoa wito kwa wananchi wasividharau virusi vya corona, bali waendelee kuchukua tahadhari ya kujikinga pamoja na kufuata maelekezo ya serikali, kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kuvaa barakoa kwenye mikusanyiko ya watu wengi na kutokaa makundi ili tuendelee kuwa salama," alisema Makala.

Alivitaja vifaa ambavyo wamevitoa kwa wakuu wa majimbo na wachungaji wa kanisa hilo kuwa ni barakoa, sabuni pamoja na vifaa vya kisasa vya kunawa mikono kwa maji tirika bila ya kugusa koki ya maji wala sabuni.

Naye Mchungaji Patrick Zengo wa Usharika wa Kanani KKKT Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alishukuru kupatiwa vifaa hivyo, ambavyo vitawasaidia kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona kwa waumini wao.

## WAGOMBEA LUKUKI

Ukurasa 13






siasa
JUMATANO JUNI 24, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

Ukurasa 12

## Ubinafsi unavyokwaza muungano wa upinzani

# Mchujo Z'bar uwaangalie wenye historia kutegemeza Muungano

**Na Ani Jozeni**

MAKADA waandamizi na wengine wanaendelea kuchukua fomu kwa kasi kutafuta saini za wanachama wa CCM wanaoweza kuwaunga mkono kuwania uteuzi kugombea nafasi ya urais kisiwani Zanzibar.

Kujitokeza makada wengi kiasi ni kuamini kuwa wanayo nafasi ya kufikiriwa na vikao husika, kuwa hakuna yeyote ambaye wote wanadhani awaye ndiye.

Kwa njia moja au nyingine, kupatikana kwa mgombea urais wa chama tawala ndiyo kielelezo cha utamaduni wa siasa uliopo nchini, kwani kupatikana kiongozi ajaye ni hatua muhimu ya kujenga uhai wa chama miongoni mwa watu. Mgombea anayeungwa mkono na sehemu kubwa zaidi ya wapiga kura analeta pumzi mpya katika chama na mwenye kuleta vikwazo maeneo mengi anarahisisha kazi ya wapinzani kuteka ngome za chama tawala pale wakuu wa kijadi na wapika maoni tofauti wakianza kumpaka matope na kuonyesha udhaifu wake. Chama lazima kihakikishe mgombea anakubalika kote.

Ila chama hakifanyi tu kazi ya kumtafuta mtangaza nia anayekubalika zaidi miongoni mwa wapiga kura, kwani anaweza akawa anakubalika kwa sababu ambazo ni hasi kwa chama, siyo sababu zote za umaarufu wake ila baadhi. Ina maana mtu kama huyo anajua anayo 'makandokando'ambayo ni hasi kwa chama, aonyeshe utii wa juu juu kwa chama ili apate uteuzi, halafu mwelekeo huo hasi uwe ni utambulisho wake miongoni mwa wananchi, na wakati huo yuko madarakani tayari.

Hakuna wakati ambao chama kimepoteza mvuto kutokana na kuwapo kiongozi ambaye hapendwi na watu, lakini baadhi ya viongozi wanaopendwa na watu wakaondolewa katika kinyang'anyiro iwe ni kwa sababu chama kinahofia sababu za kupendwa kwao, wamekisumbua chama. Ndiko wanakotokea baadhi ya viongozi mashuhuri wa upinzani, kwa mfano Seif Shariff Hamad maarufu Maalim Seif, Augustine Mrema, na kwa uchaguzi mkuu uliopita Edward Lowassa. Uteuzi wa mgombea kwa uchaguzi wa rais ni mwanzo wa kupata kiongozi mpya katika CCM iwe ni Muungano au Visiwani, ila mara nyingi ni fursa nyingine kwa upinzani kupata kada mahiri kutoka chama tawala, kusaidia kubomoa ngome za chama tawala.




Mbio zimeanza kuwarithi Dk. Ali Mohamed Shein (kushoto) na makamu wake Balozi Seif Ali Iddi. **PICHA MTANDAO.**

**URAIS ZANZIBAR**

Kila unapowadia wakati wa kutafuta mgombea kwa urais kwa CCM, ipo hali ya kisiasa inayotawala wakati huo na inachangia kwa kiasi kikubwa kujua nani anafaa kushika bendera na kuogoza kipindi kinachofuata. Katika wakati huu hakuna ugomvi wa wazi kati ya makada wa CCM Zanzibar na uongozi wa serikali ya Muungano kwani sehemu kubwa ya 'kero za Muungano' ilitatuliwa kutokana na maazimio ya Bunge Maalum la Katiba.

Wapo wanaongojea kukamilishwa kwa mchakato wa Katiba Mpya kwa vile tu wanaipenda iwe mpya, ila serikali ya awamu ya nne ilitumia mkutano ule wa kitaifa kutafuta muafaka kwa masuala ambayo yameutesa Muungano kwa miongo mitano na kwa jumla ulifanikisha zoezi hilo.

Uteuzi wa kwanza wa mgombea urais Zanzibar wakati wa vuguvugu la vyama vingi, mwaka 1985 ndiyo uliweka msingi wa eneo moja muhimu la utamaduni, kuwa vijana wanawapisha wazee. Maalim Seif wakati huo alikuwa kijana, akaambiwa na Mwalimu Julius Nyerere Raia wa Tanzania, ampishe Idris Abdulwakil, akabisha na kukataa. Ndiyo alivyohamia upinzani na hata akipata kura nyingi.

Ni kanuni hiyo pia ilitumika katika kumpata mgombea mwaka 1995 kwa upande wa jina la mgombea wa CCM urais Muungano, ambako Jakaya Kikwete aliongoza kwa kura, Mwalimu akambwambia ampishe Benjamin Mkapa (anayemzidi umri kwa miaka 12), na Mungu akipenda atapata nafasi baadaye, na ndivyo ilivyokuwa.

Ila miaka 10 kabla ya hapo, mwaka 1985 kuna kitu kama kanuni kilichowekwa na sasa kinaweza kuonyesha mwelekeo wa uteuzi wa mgombea urais Zanzibar. Mwalimu alipendekeza jina la Salim Ahmed Salim, wakati huo akiwa Waziri Mkuu, wajumbe wakamuunga mkono ila kwa tahadhari moja, akaulizwa 'kwani makamu wetu ana tatizo gani?' Wakimaanisha kwanini asiwe Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye alikuwa Ali Hassan Mwinyi, wakati huo akiwa Rais wa Zanzibar, badala yake awe mwanadiplomasia Salim Ahmed Salim.


**HISTORIA KUJIRUDIA?**

Ndiyo maana kuna uwezekano wa kutokea mazingira kama hayo, kuwa yako majina kadhaa ambayo yamezoeleka midomoni mwa watu, kuwa ni viongozi shupavu na mahiri, wakitazamia kuwa mmojawapo ndiye anafaa, au tayari wana jina lake. Si ajabu mwenyekiti wa kamati ndogo ya Kamati Kuu ya CCM kwa upande wa Zanzibar, au Sekretariati ya CCM Zanzibar aje na jina linapopendekezwa upande huo kama ilivyotokea mwaka 2005.

. Kanuni hiyo ni wazi kuwa itakumbukwa kwa hiyo Zanzibar hawatakuja na jina ila majina, na yatakapojadiliwa Kamati Kuu, atakayekuwa anapendekezwa iwe na Zanzibar au na baadhi ya wajumbe itabidi ajibu swali la 1955 pia.

Kuna eneo jingine ambalo linaweza kumsaidia 'Makamu Wetu' kupeta katika kinyang'anyiro hicho, kuwa kukabidhi mikoba ya ngazi ya urais Zanzibar kwa makamu itakuwa ni hatua itakayopendezesha chama katika kukubalika kwake na sehemu tofauti za jamii. Itakuwa ni hatua nyingine ya kujivunia kujenga jamii yenye usawa na hasa katika eneo la jinsia, hivyo wagombea au watangaza nia wengine watakuwa na kazi ngumu kumpangua 'Makamu Wetu.' Labda wangemwomba sana akatae mwito wa kuchukua hizo fomu ambao pengine ameshaupokea.

# Ubinafsi unavyokwaza muungano wa upinzani



Edward Lowassa



Augustine Mrema

**Na Mashaka Mgeta**

KWA zaidi ya muongo mmoja sasa, suala la vyama vya wapinzani kuunganisha nguvu ili kuviondoa vilivyopo madarakani hasa barani Afrika limekuwa la kipaumbele lakini pasipo kuwa na mafanikio endelevu.

Kadhalika hapa nchini, muungano kama huo si jambo geni. Ulijitokeza wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, wakati vyama vya Chadema, NCCR-Mageuzi, CUF na NLD vilipounganisha nguvu zao kupitia mwamvuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

Uchambuzi unaofanywa katika siasa za mataifa kadhaa, unadhihirisha kuwapo kasoro mbalimbali zinazovikwamisha vyama hivyo kuwa imara na kuziondoa madarakani serikali za nchi zao. Hali kama hiyo ipo Tanzania, ambapo tangu kuingia kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, na baadaye uchaguzi mkuu wa kwanza uliovishirikisha vyama hivyo mwaka 1995, hisia za wapinzani kuunganisha nguvu zao zilitokea. Lakini hawakufanikiwa.

Ndiyo maana haikushuhudia ukiungana mwaka 1995 wakati aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri Mkuu (pamoja na nyadhifa nyingine), Augustine Mrema alitoa ushindani mkubwa katika uchaguzi huo.

Akiwania kupitia chama chga NCCR-Mageuzi, Mrema alipata kura 1,808,516 sawa na asilimia 27.77 nyuma ya aliyeongoza, Benjamin Mkapa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) aliyepata kura 4,026,422 sawa na asilimia 61.82 na wagombea wengine walipata chini hapo.

Mrema alizichukulia kura hizo kama mtaji wa kuingia nao kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, lakini hali ikawa tofauti na matarajio yake, akaambulia kushuka na kushika nafasi ya tatu nyuma ya Mkapa na Profesa Ibrahim Lipumba wa CUF.

Hivi sasa Mrema hana matarajio ya kuwania nafasi hiyo ya juu kabisa katika utawala wa nchi, badala yake ni kama amenyanyua mikono, akisimamia ukweli anaouamini kwamba 'Rais John Magufuli anatosha 2020".

Mwanasiasa huyo aliyevuma sana katika siasa za upinzani kwenye miaka ya mwishoni mwa 1990, bado anaiongoza Tanzania Labour Party (TLP) aliyokabidhiwa na aliyekuwa mtangulizi wake, Leo Lwekamwa.

Hata ulipofanyika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, wakati huo CUF ikiwa na nguvu kubwa kwa vyama vya upinzani, hoja ya wapinzani kuungana ilizungumzwa pasipo kufikiwa.

Kisha kila chama kikaingia kwenye uchaguzi na kama ilivyotarajiwa, Rais (mstaafu) Mkapa akaongoza kwa kura 5,863,201 (sawa la asilimia 71.74) akifuatiwa na Profesa Lipumba wa CUF aliyepata kura 1,329,077 (asilimia 16.26 na Mrema akaambulia kura 637,077.

Mwaka 2005, mambo yalibadilika katika kuwania nafasi hiyo ambapo Chadema ambayo mwaka 1995 na 2000 haikumsimamisha mgombea ubunge, ilimteua Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe kuisaka Ikulu dhidi ya aliyekuwa mgombea kupitia CCM, Jakaya Kikwete.

Matokeo ya uchaguzi huo ulioguswa pia na minong'ono ya wapinzani kuunganisha nguvu zao, yalimpa ushindi Kikwete aliyepata kura 9,123,952 (sawa na asilimia 80.28) akifuatiwa na Profesa Lipumba (CUF) - kura 1,327,125 sawa na asilimia 11.68, Freeman Mbowe (Chadema) - kura 668,756 sawa na asilimia 5.88 na Mrema (TLP) kura kura 84,901 sawa na asilimia 0.75.

Mwaka 2010, kama ilivyokuwa kwa uchaguzi mkuu uliopita, vyama kadhaa vya upinzani vikashiriki mazungumzo ya kuunda muungano usio rasmi, lakini hakuwezekana na badala yake Chadema ikaingia ikiwa na nguvu kubwa hasa baada ya kumsimamisha aliyekuwa Katibu Mkuu wake, Dk Wilbroad Slaa.

Kikwete wa CCM alishinda kwa kupata kura 5,276,827 - sawa na asilimia 61.17, akifuatiwa na Dk Wilbrod Slaa (Chadema) kura milioni 2.2 sawa na asilimia 26.34 na Profesa Lipumba wa CUF kura 695,668, sawa na asilimia nane. Wagombea wengine walipata chini ya hapo.

Nia ya kuwapo muungano wa wapinzani ikatimia mwaka 2015. Vyama vya upinzani vikisukumwa na kasoro walizozibaini kwenye Bunge la Katiba, wakajikuta wanasimama pamoja na kuunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

Katika uchaguzi huo, Rais mstaafu Kikwete alikuwa anamaliza muda wake wa utawala na hivyo, nchi ilikuwa inaelekea kumpata rais mpya wa awamu wa tano.

CCM ilidaiwa iligawanyika kimtazamo kama ilivyo kwa chama tawala katika nchi yoyote ambapo rais aliyepo anaondoka madarakani.

Ni mgawanyiko uliotafsiriwa kuwa mkubwa kutokea ndani ya CCM tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi, ukishuhudia waliowahi kuwa mawaziri wakuu, Edward Lowassa na Frederick Sumaye wakihamia Chadema.

Katika kuhama huko, Lowassa aliyekuwa ameimarisha kambi yake ndani ya CCM, alipewa fursa ya kuwania urais kupitia Chadema, akiungwa mkono na Ukawa. Hata hivyo, pamoja na kampeni zake kusheheni umati mkubwa watu, alishindwa na CCM, Rais John Magufuli.

Katika Uchaguzi Mkuu huo wa 2015 ambao upinzani ulionyesha kupata nguvu zaidi kwa mgombea urais wake, Lowassa alipata kura 6,072,848 ikiwa ni asilimia 39.97, akiwa nyuma ya mshindi, Rais Magufuli wa CCM aliyepata kura 8,882,935 ikiwa ni asilimia 58.46

Said Salim ni mchambuzi wa masuala ya siasa akiwa Unguja-Zanzibar anaiambia Sauti ya Ujerumani -DW kuwa msingi wa muungano wa vyama wakati wa uchaguzi mkuu una lengo jema la kufanikisha kuziondoa madarakani serikali zilizoshindwa kuwajibika ipasavyo kwa umma.

Hata hivyo, Salim anasema kwa hali inayojitokeza hususani Tanzania, muungano wa wapinzani unakuwa mfano wa kile alichokiita "mchezo wa kitoto" ulioghubikwa na maslahi binafsi. Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba vyama vya upinzani vinachelewa kuunganisha masuala yanapaswa kuwa katika umoja wao, badala yake kuibuka muda mfupi inapokaribia uchaguzi mkuu.

"Wanapokaribia kipindi cha uchaguzi ndipo wanapoibuka na kwa sababu hawana mambo ya msingi ya muda mrefu yanayowaunganisha, utawakuta wanagawanyika na kuendelea kuwakatisha watu tamaa," anasema.

Mchambuzi huyo anahoji ikiwa wapinzani katika kuungana kwao, wamekuwa na nia ya dhati ama ni matokeo ya kutaka kukidhi 'njaa' ambayo hata hivyo hakuifafanua.

Anasema manufaa ya muungano wa wapinzani na uwezekano wa kufikia lengo la kuwatoa watawala madarakani, litafanikiwa ikiwa wanasiasa wataweka kando ubinafsi na kushughulikia masuala yenye tija kwa umma.

Anasema pamoja na changamoto zinazowakabili, muungano wa wapinzani umeonyesha mafanikio katika nchi kadhaa za Afrika ikiwamo Tanzania.

Hata hivyo, anasema katika hali inayoonekana kukosekana umakini wa kutosha, tayari Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amekaririwa akilalamika kuwa Chadema haikutekeleza makubaliano yakiwamo kuvigawia ruzuku vyama vilivyounda Ukawa.

Inavyoonekana muungano wa wapinzani nchini hauna tija sana kama ilivyo kwa nchi nyingine za Afrika, kutokana na uimara wa CCM iliyojikita katika eneo kubwa la nchi.

Mchambuzi wa masuala ya siasa wa nchini Kenya, Profesa Hermani Manyora, anasema hatua ya vyama vingi kuungana hakutokani na kuwa na itikadi na falsafa zinazofanana, bali wanachokitaka ni kutwaa uongozi.

Profesa Manyora anasema kutokana na hali hiyo, vyama hivyo vimejikuta vikishindwa kufikia malengo ya kupata ushindi ama kusambaratika mapema kwa vile vinavyofanikiwa kuingia Ikulu.

Anatoa mfano wa uchaguzi mkuu wa Kenya mwaka 1992 ambapo wapinzani waliungana kupitia FORD vikatawanyika na Rais wa wakati huo, Daniel Moi (marehemu) akashinda.

Pia anasema baada ya muda wapinzani waliungana tena nchini humo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2002, sababu kubwa ikiwa ni kupinga hatua ya aliyekuwa Rais wa Kenya, Moi kumchagua Uhuru Kenyatta kuwania urais kupitia chama cha KANU.

Anasema kilichowaunganisha wapinzani hao wakiwamo waliotoka katika KANU haikuwa itikadi ama falsafa zinazofanana, bali hasira zao dhidi ya hatua ya Moi kumteua Kenyatta.

Hata hivyo, Profesa Manyora anasema muungano wa vyama vya upinzani una manufaa kwa nchi za Afrika hasa zile zinazoongozwa na serikali zilizokithiri kwa ufisadi na ukiukwaji wa haki za binadamu.

**Maoni 754 691540, mgeta2000@yahoo.com.**

# WAGOMBEA LUKUKI

## • Ni kujifunza kutokana na makosa
## • Kuimarika demokrasia ya ndani

**Na Sabato Kasika**



Mchungaji Peter Msigwa



Dk. Rose Mary Majige

WANACHAMA 11 wamejitokeza katika mchakato wa ndani wa watia nia ya kuki-wakilisha Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), katika kuwania urais kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Wanachama hao wenye nia ya kupeperusha bendera ya Chadema ni Freeman Mbowe, Tundu Lissu, Isaya Mwita, Mchungaji Peter Msigwa, Lazaro Nyalandu, Nicodemus Gasper, Dk. Maryrose Majinge, Shaban Msafiri, Richmund Simba, Manyama Leonard na Naro Opiyo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene, wanachama 11 ndiyo waliokidhi vigezo vya awali vya kutia nia kwa mujibu wa katiba ya chama hicho.

Hatua hii ya kuruhusu wanachama kujitokeza kutia nia ya kuwania urais imekuwa tofauti na uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ambapo chama hicho kibadili gia angani na kumpendekeza Edward Lowassa kuwania nafasi hiyo.

Lowassa ambaye ni Waziri Mkuu mstaafu, alipendekezwa kuwania nafasi hiyo baada ya kutoka CCM kutokana na jina lake kukatwa kwenye wagombea wa urais na kutoswa katika mchakato wa chama hicho wa kumpata mgombea.

Hata hivyo, hatua ya kumpendekeza Lowassa kuwania urais, ilizua sintofahamu ndani ya Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) na kusababisha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Willbrod Slaa, kukimbia na kuhamia CCM.

Wakati Dk. Slaa akihamia CCM, mwanasiasa mwingine, Prof. Ibrahim Lipumba, aliachia nafasi ya uenyekiti ndani ya Chama cha Wananchi (CUF), sababu kuu ikiwa ni Lowassa na kuruhusiwa kuwania urais.

CUF, Chadema, NCCR -Mageuzi na NLD, vilikuwa vimeunda Ukawa, ambao uliviwezesha kugawana baadhi ya majimbo na kata kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Pamoja hayo, kasoro iliyojitokeza ni kusababisha baadhi viongozi wa vyama hivyo kujitoa, ni hiyo ya kumpitisha Lowassa kugombea urais huku wanachama wengine waliotaka nafasi hiyo kuachwa, hata hivyo amerejea katika chama hicho tawala na kuendelea na maisha ya kisiasa.

### UCHAGUZI MKUU 2020

Katika uchaguzi mkuu ujao, hali imekuwa tofauti, kwani wamejitokeza wananchi wengi waliotia nia kwa ajili kuomba ridhaa ya chama kuwapendekeza kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kutokana na wingi huo wa wanachama kutia nia, baadhi ya wachambuzi wa siasa nchini wametoa maoni yao, kwa nini kwa mara ya kwanza imekuwa hivyo ndani ya Chadema.

Said Msonga, ni mchambuzi anayezungumza na Nipashe akisema kwamba, Chadema imejifunza kutokana na makosa na sasa haitakiwi kuyarudia tena.

"Kama unakumbuka, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Chadema ilimsimamisha Edward Lowassa kuwania urais, lakini baadaye akawaacha kwenye mataa kwa kurudi CCM," anasema Msonga.

> Ninajua kwamba vyama vya upinzani vimekuwa katika mazingira magumu, havikuwa na muda wa kukutana na wanachama au Watanzania na sijui kama muda wa kampeni utavitosha kujinadi kikamilifu," anasema Msonga.

Anaeleza kuwa kutokana na hali hiyo, chama kitakuwa kimejifunza na kuamua kufungua milango wazi kwa wanachama wenye uwezo wa kuwania nafasi hiyo ili watie nia badala ya kumwachia mwanachama mmoja kama ilivyokuwa kwa Lowassa.

"Chadema kama taasisi kimefuangua milango kwa wanachama wote wenye sifa, hivyo hatua hiyo izingatie katiba, kwani inaweza kuwa imesaidia kurudisha imani kwa wanachama watiifu," anasema.

Mchambuzi huyo wa siasa, anaongeza kuwa chama hicho kimejifunza na sasa kimerejea kwenye mstari, na kwamba kilichobaki ni kuheshimu na kuiachia demokrasia ifanye kazi na haki itendeke.

Aidha, anasema, kujitokeza kwa wanachama wengi kuwania urais ni dalili kwamba chama hakikosi umaarufu licha ya kuondokewa na baadhi ya wanachama na viongozi wakiwamo wabunge na madiwani.

"Ninajua kwamba vyama vya upinzani vimekuwa katika mazingira magumu, havikuwa na muda wa kukutana na wanachama au Watanzania na sijui kama muda wa kampeni utavitosha kujinadi kikamilifu," anasema Msonga.

Anaongeza kuwa inabidi vifanye kazi ya ziada kufikia wananchi ili hata kama havikushinda, vitakuwa vimerudisha imani kwa wanachama na mashabiki wa siasa za Tanzania.

### KUIMARIKA KISIASA

Wakati akisema hayo, mchambuzi mwingine, mwanazuoni Abbas Mwalimu, anasema kujitokeza kwa wanachama wengi kutia nia ya kuwania urais, ni dalili za kuimarika kwa siasa za ndani ya chama hicho.

Mbali na hilo, Mwalimu anasema, sababu nyingine ya kujitokeza kwa wanachama wengi, inaweza kuwa ni kuwapo kwa makundi yasiyoaminiana ndani ya chama, ambayo kila moja linataka mtu wake awanie nafasi hiyo.

"Hivyo ndivyo ninavyoutazama wingi huo wa wanachama wa Chadema waliojitokeza kutia nia ya kugombea urais katika maeneo mawili, ambayo ninaamini ndivyo ilivyo, kwani ndivyo ilivyo," anasema Mwalimu.

Anasema, ni wakati wa Chadema kuwa makini katika kutafuta jina la mwanachama atakayepeperusha bendera ya chama katika uchaguzi mkuu bila kuacha mpasuko unaotokana na makundi. "Njia ya kuepusha mpasuko au mgawanyiko, katika mchakato huo, ni kuendesha mambo kwa uwazi, na kuzingatia katiba, sheria, kanuni na taratibu ambazo chama kimejiwekea," anasema.

Mwalimu anasema, demokrasia imechukua mkondo wake kwa kuruhusu watia wengi ili wachuane na kwamba hali hiyo ikiendelea hadi mwisho wa mchakato, hakuwezi kutokea mgawanyiko.

# Wapigakura mnaitumiaje haki yenu ya kutoa maoni?

Na Mwandishi Wetu

OKTOBA, mwaka huu Tanzania inafanya uchaguzi mkuu kama ambavyo inaelekezwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 76(1) inayosema: "Kila baada ya bunge kuvunjwa kutakuwa na uchaguzi wa wabunge katika majimbo yote ya uchaguzi".

Uchaguzi huo huenda pamoja na wa rais na madiwani na hicho ndicho kinachongojewa kitokee kwani bunge limeshavunjwa tangu Jumanne iliyopita Juni 16 na mchakato wa kuchukua fomu umeshaanza.

Aidha, kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 20(1) inasisitiza kuwa kila mtu anastahili kuwa huru bila ya kuathiri sheria za nchi kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika na kushirikiana na wengine, kutoa mawazo hadharani na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi ya wengine. Ndivyo katiba inavyowaruhusu Watanzania kuwa wanachama wa vyama vya kisiasa vya kiraia na vingine kwa lengo la kutimiza haki ya kukusanyika na kukusanyikana na jumuiya anazozipenda.

Katika kuhakikisha kuwa kila mmoja anasikika, katiba hiyo kwenye ibara ya 18 inawapa wananchi uhuru wa kutoa maoni ndiyo maana wakati huu wapigakura na watiania kwenye ubunge , udiwani na urais wanapolisogelea sanduku la kura, huu ndiyo muda wa wapigakura kutumia uhuru wa kutoa maoni , kuhoji na kuzikagua ahadi zilizotolewa kwenye ilani za vyama na washirika wao katika kuwahudumia wananchi.

Hiki ndicho kipindi ambacho wananchi wanapotekeleza ibara ya (76) 1 wanahitaji kutumia uhuru wa kutoa maoni ambao ni muhimu muda wote katika utawala wa kidemokrasia lakini zaidi sana wakati huu wa uchaguzi mkuu.


Ndiyo muda wa wapigakura kuikagua serikali na pia vyama vyao kupitia wabunge , madiwani na kuzichunguza ilani zake na kuhoji iwapo kile walichoahidiwa kwenye jukwaa la kuomba kura miaka mitano iliyopita kimetimizwa.

Wananchi wanatakiwa kuutumia uhuru wa kukosoa pale wanapofikiri kuna matatizo yanatokea. Kwa mfano kuna sehemu ambazo huduma za maji hazipatikani na kipindi cha corona ingekuwa changamoto kubwa, lakini cha kushukuru ni kwamba ulikuwa msimu wa mvua.

Kwa mfano, wakazi wa Mbezi Msumi jijini Dar es Salaam, wanaishi eneo ambalo halina maji ya bomba yanayosambazwa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (Dawasa) kwa miaka mingi.

Baadhi wakizungumza na gazeti hili kuhusu uhuru wa kutoa maoni kuelekea uchaguzi mkuu, wanasema kwa kipindi kirefu wameshuhudia vifo vya watoto

> Kwetu sisi. Wakati wa uchaguzi ni muhimu kuutumia uhuru wa kutoa maoni kuisema serikali na kuieleza tatizo hili kwani ni changamoto inayotuumiza zaidi. Ni wakati wa kujadili namna mambo yalivyofanyika, kubainisha na kuainisha shughuli nyingine zilivyokwama na namna changamoto hizo zinavyoweza kusahihishwa." Anasema mmoja wa jamaa wa Mbezi Msumi ambaye familia yao ilimpoteza ndugu yao aliyezama kwenye madimbwi ya maji yaliyoko eneo la Kwa Binti Mbingu miaka mwili iliyopita.




kutumbukia kwenye visima vya maji vya kuchimbwa na pia kwenye madimbwi ya maji yaliyotuama.

Maji hayo yanatuama kutokana na sehemu hizo kuchimbwa mchanga na sasa ni mabwawa makubwa yanayojaa maji na kusababisha vifo vya watoto, wanyama na hata watu wazima hasa wanaokatisha maeneo hayo wakiwa wametumia kilevi.

"Kwetu sisi. Wakati wa uchaguzi ni muhimu kuutumia uhuru wa kutoa maoni kuisema serikali na kuieleza tatizo hili kwani ni changamoto inayotuumiza zaidi. Ni wakati wa kujadili namna mambo yalivyofanyika, kubainisha na kuainisha shughuli nyingine zilivyokwama na namna changamoto hizo zinavyoweza kusahihishwa." Anasema mmoja wa jamaa wa Mbezi Msumi ambaye familia yao ilimpoteza ndugu yao aliyezama kwenye madimbwi ya maji yaliyoko eneo la Kwa Binti Mbingu miaka mwili iliyopita.

Anaeleza kuwa ni kaka yake aliyefariki baada ya kuingia majini kumuokoa mtoto aliyekuwa anafua jirani naye wakati kijana huyo anasafisha pikipiki yake.

"Ndugu yangu alikuwa bwawani hapo anaosha bodaboda na hatua chache alikuwapo mwanafunzi wa darasa la pili anafua nguo. Akasikia kishindo cha kuzama

> Wanawake wasikae kimya, wakisubiri kuwa kuna watu watakaowasemea. Ni wakati wa kutoa maoni yao na kueleza kuwa wanataka kugombea nafasi mbalimbali.

majini na akaharakisha kumuokoa mtoto huyo. Lakini wote walinasa kwenye tope na kupoteza maisha. Licha ya kwamba miili yao iliopolewa. Haya yasingetokea kama mbunge, diwani na serikali zingesaidia eneo hili kupata huduma ya maji..." anasema kijana huyo akiomba asitajwe jina.

Anaeleza kuwa katika kipindi hiki ndiyo muda muafaka wa kutumia uhuru wa kutoa maoni kuijadili na kuipima serikali kwa kuangalia kile wabunge na madiwani na taasisi za umma zilichofanya.

Anaongeza kuwa ndiyo muda mwafaka kwa wale wanaoongoza mjadala wa kuja kuomba kura kueleza bayana ni wapi serikali haikutatua changamoto na kitu gani kifanyike ili kurekebisha tatizo na kasoro hizo.

Kwa upande mwingine wakati huu wa kampeni za uchaguzi ni muda mwafaka kwa serikali kueleza ni namna na kiasi gani imetekeleza ahadi zilizotolewa huko nyuma wakati wa kuomba ridhaa ya kuongoza taifa.

Lakini pia, ndiyo muda wa wananchi kutoa maoni yao kwa serikali ili ijibu tuhuma na hoja zinazotolewa dhidi yake.

**KAZI IANZE SASA**

Akizungumzia umuhimu wa kutoa maoni wakati huu wa uchaguzi Mkurugenzi wa Chama cha Wanawahabari Wanawake (Tamwa), Rose Reuben, anasema ni muhimu kutoa maoni ili kuangalia ushirikishwaji na utekelezaji wa masuala ya kimaendeleo iwapo yamefanywa kwa mrengo wa kijinsia.

Anaongeza kuwa wanawake wanatakia kuwa mstari wa mbele kuuliza, kuhoji, kuchambua na kutoa maoni yao kuhusu maandalizi ya ilani za vyama, taratibu za kugombea na jinsi uchaguzi wa viongozi utakavyoleta matokeo yanye usawa wa kijinsia.

"Wanawake wasikae kimya, wakisubiri kuwa kuna watu watakaowasemea. Ni wakati wa kutoa maoni yao na kueleza kuwa wanataka kugombea nafasi mbalimbali.

"Kufanya hivyo ni kutaka kuona taratibu zinazowawezesha kupendekezwa kugombea ubunge na udiwani kwenye majimbo na viti maalumu zinabainishwa na kuwekwa wazi. Waanze kutoa maoni yao sasa. Watumie haki yao ya kidemokrasia si kusubiri mpaka hatua za mwisho mambo yameshapangwa na kukamilika," anashauri Rose.

Ni muda ambao wanawake wanatakiwa kutoa maoni na kutumia vyombo vya habari kuhamasisha masuala ya kushirikiana na kuungana mkono. Kuunga mkono wagombea wanawake kwa hali na mali ili kufanikisha kuwa na uongozi unaochaguliwa kidemokrasia wenye kuwashirikisha wanawake, watu wenye mahitaji maalumu, wazee na vijana.

Anasema kutumia uhuru wa kutoa maoni na kufuatilia kinachoendelea kwenye mchakato wa uchaguzi kianze sasa badala ya kusubiri mpaka hatua za mwisho.

Wanawake wanatakiwa kuhoji ilani zinazungumzia vipi usawa wa kijinsia? Uteuzi shirikishi kati ya wanawake na wanaume kwenye majimbo umewekewa uwiano na utaratibu shirikishi?

Ni wazi kuwa baada ya kulumbana, kuhoji, kupendekeza na kukosoa kazi inabakia kwa waamuzi au majaji ambao ni wananchi na watatoa uamuzi kwenye sanduku la kura.





# ‘Corona isiwe kigezo watoto kukosa chanjo’

**Na Agusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeitaka jamii kuhakikisha watoto wanapata chanjo kipindi hiki chenye maambukizi ya virusi vya corona (Codid-19) ili wapate kinga ya magonjwa mengine.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma ya Afya ya Uzazi na Watoto, Dk. Ahmad Makuwani, kwenye semina ya waandishi wa habari wa mikoa ya Singida na Dodoma kuhusu chanjo.

Alisema maambukizi ya corona kwa sasa yamepungua na kuwataka Watanzania kutotumia ugonjwa huo kama sababu ya kutowapeleka watoto kupata chanjo.

“Tulikuwa tunaenda vizuri, lakini hivi karibuni idadi ya watoto na wasichana wanaopaswa kupata chanjo ya mlango wa kizazi imepungua, hizi chanjo ni muhimu sana jamii ipeleke watoto kwenye vituo wapate chanjo,” alisema.

Alisema Tanzania imepiga hatua kwa sasa katika utoaji wa huduma za chanjo, huku akidai kuwa kuna vituo zaidi ya 6,000 vinavyofanya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi.

“Tunaamini mtatumia weledi wenu kuelimisha jamii kuhusu huduma ya chanjo mbalimbali zinazotolewa, wahimizeni wananchi kule vijijini wapeleke watoto wao kwa kuwa chanjo inatolewa kwenye vituo vya kutolea huduma,” alisema.

Alisisitiza kuwa waandishi kuendelea kuhamasisha wananchi kunawa mikono kwa kuwa imesaidia kuondokana na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu.

Awali, akizungumzia hali ya huduma za chanjo nchini, Ofisa Programu wa chanjo katika Mpango wa Taifa wa Chanjo kutoka Wizara ya Afya, Lotalis Gadau, alisema pamoja na jitihada za kuhakikisha magonjwa yanayozuilika kwa chanjo yanapewa kipaumbele kwa kuwapatia watoto, lakini bado kuna jamii hazichanjii watoto wao.

“Kuwapo kwa ugonjwa wa corona sio sababu ya kutopeleka watoto kupata chanjo kwa sababu wakichanjwa inasaidia kuwakinga na magonjwa mengi zaidi,” alisisitiza.

Alisema chanjo ya surua, rubella na HPV ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi uchanjaji wake upo kwa kiwango cha chini na kuwataka waandishi wa habari kuhamasisha jamii.

# Watakaovuruga uchaguzi mkuu CCWT waonywa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Wafugaji Tanzania (CCWT), kimesema kitahakikisha kinamchukulia hatua mtu au kikundi chochote kitakachokwamisha uchaguzi wa viongozi wa chama hicho unaotarajiwa kufanyika Julai 16, mwaka huu.

Onyo hilo lilitolewa na Katibu wa CCWT Taifa, Magembe Makoye, alipokuwa akizungumza na Nipashe jijini Dodoma.

Alisema kumeibuka vikundi kadhaa vikitoa kauli mbalimbali zinazolenga kukwamisha uchaguzi huo, na kusisitiza kuwa watahakikisha wanashirikiana na serikali ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

“Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa chama chetu, nitoe wito kwa wafugaji kujiandaa kushiriki uchaguzi huu ama kujitokeza kugombea na kuchagua viongozi, wale wote waliojiandaa kufanya kampeni kwa kuwachafua wenzao au kutumia rushwa watashughulikiwa,” alisema.

Alisisitiza kuwa vitendo vyovyote vya uvunjifu wa amani na sheria vitachukuliwa hatua kali kwa yeyote atakayetenda.

Aliwaomba wafugaji na wanachama wa chama hicho kulipa ada zao za mwaka mapema kabla ya mkutano ili kuepuka usumbufu utakaojitokeza siku husika.

“Ada zinazotakiwa kulipwa zipo kwenye Katiba yetu, ambapo kifungu cha sita kinataja kiwango na kiingilio ni Sh. 50,000, na nitoe wito kwao kushiriki uchaguzi huu ili kuchagua viongozi wanaowataka wawaongoze,” alisema.

Hata hivyo, alisema chama hicho kipo salama na taarifa za tishio la kufutwa zilitokana na kukosekana kwa mawasiliano kati yao na viongozi wa serikali, lakini kwa sasa utata huo haupo.

“Sisi viongozi wa chama tutaendelea kutoa ushirikiano na uwezeshaji wowote utakaohitajika kufanikisha uchaguzi wetu utakaofanyika Dodoma na utatanguliwa na mkutano wa maandalizi utakaofanyika Juni 25, mwaka huu,” alisema.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa CCWT Mkoa wa Dodoma, Reginald Lubeleje, alilalamikia kuwapo kwa masharti kwa wajumbe wa mkutano wa uchaguzi ambayo hayapo kwenye Katiba yao.

“Kwenye barua zinasema lazima mjumbe awe amelipa ada ya mwaka Sh. 50,000, hili siyo kweli hata kidogo, sisi tunalipa kiasi hicho kama kiingilio na mwanachama akishalipia kiasi hicho basi kila mwaka anatakiwa kulipa Sh. 5,000 tu,” alisema.

Alibainisha kuwa wanaona kuwa uchaguzi wa chama hicho umeanza kuingia mizengwe ambayo inakinzana na katiba yao waliyonayo kwa sasa.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Msalato, jijini Dodoma wakimsikiliza mwalimu wao (hayupo pichani) shuleni hapo jana, yakiwa ni maandalizi ya kujiandaa na mitihani yao inayotarajiwa kuanza mwisho wa mwezi huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Jafo aagiza tathmini ya miundombinu ya shule

**Na Augusta Njoji,** BAHI

WAKUU wa mikoa, wilaya na wakurugenzi nchini wametakiwa kufanya tathmini ya kina ya miundombinu mibovu kwenye shule na kufanyia ukarabati.

Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alipokuwa akizindua Shule ya Sekondari Nondwa na kupokea meza 45 na viti 75 vya Shule ya Sekondari Ibihwa wilayani humo vilivyokarabatiwa na Taasisi ya Msuya Foundation.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kuweka utaratibu wa kubaini hali ya miundombinu ya shule na kufanyia ukarabati samani zilizoharibika ili kuokoa fedha ambazo zingetumika kununua mpya.

“Taasisi nyingine zinapaswa kuiga mfano wa taasisi hii ili kuendelea kutatua changamoto zilizopo kwenye sekta ya elimu,” alisema.

Akizindua Shule ya Nondwa, Jafo aliagiza shule hiyo kuanza kutumika Juni 29, mwaka huu ili wanafunzi waondokane na kutembea umbali wa kilometa 15 kusoma katika kata ya Chikopelo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Ombeni Msuya ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), alisema taasisi hiyo ilifanya utafiti wa hali ya miundombinu mwezi Februari mwaka huu na kutumia matokeo yake kufanya ukarabati huo.





Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia miundombinu, Elias Kwandikwa (kushoto), akipokea maelezo ya mchoro wa ramani ya jengo la abiria kutoka kwa Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Songwe (SIA) mkoani Mbeya, Pius Kazeze, alipotembelea uwanja huo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**.

# Kampuni yaagizwa kujenga uwanja usiku na mchana

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imeiagiza Kampuni ya China Geo Engineering Cooperation iliyopewa kandarasi ya kurekebisha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, kufanya kazi usiku na mchana ili kazi hiyo ikamilike kwa wakati.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia miundombinu, Elias Kwandiwa, wakati akikagua maendeleo ya mradi wa ukarabati wa uwanja wa huo.

Kwandikwa alisema licha ya kazi hiyo ipo nyuma ya wakati kutokana na muda mwingi kupotea kwa sababu ya kuibuka kwa janga la corona na mvua nyingi mwaka huu.

Alisema ili kufidia muda huo ni lazima kampuni hiyo ianze kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kazi hiyo inamalizika kwa muda uliopangwa.

"Pamoja na kwamba tunajua muda mwingi umepotea hapa kwa sababu ya mambo yaliyoibuka, lakini tunahitaji kazi hii ikamilike kwa wakati, hivyo kuanzia sasa inabidi kazi hii ianze kufanyika usiku na mchana," alisema Kwandikwa.

Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya anayesimamia mradi huo, Eliazary Rweikiza, alisema mkataba wa mradi ambao ulisainiwa mwezi Agosti mwaka jana ni wa miezi minane.

Alisema mradi huo unaigharimu serikali Sh. bilioni 14 ambazo zitafanya kazi ya kukarabati njia ya kurukia ndege, uzio wa uwanja na maegesho ya ndege zenye dharura.

Hata hivyo, Rweikiza alisema kuwa mradi huo unakabiliwa na changamoto ya mkandarasi kuchelewa kupeleka vifaa muhimu vya kazi kwenye eneo la mradi hali ambayo inasababisha mradi huo kusuasua.

Kwa upande wake Meneja wa Mradi huo, Qin Lihua, alisema baadhi ya wataalamu wake walishindwa kuingia nchini kutokana na safari za ndege kuzuiwa kwa sababu ya janga la corona.

Alisema baada ya serikali kuruhusu ndege kuingia na kutoka nchini sasa wataalamu hao wanatarajiwa kufika wakati wowote kuanzia sasa ili kukamilisha ujenzi huo na kukamilika ndani ya kipindi cha miezi nane.

# Polepole awasihi vijana wasikubali kushawishiwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIBU wa Itikadi, Siasa na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, amewataka vijana nchini wasikubali kushawishiwa na baadhi ya viongozi waandamizi waliokuwa makada wa chama hicho ambao wameadhibiwa kutokana na makosa mbalimbali ya utovu wa nidhamu ndani ya CCM.

Polepole alitoa kauli hiyo jana wakati wa mkutano wake na wanachama wa CCM wakiwamo wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu uliofanyika jijini hapa.

Alisema anashangazwa na tabia ya baadhi ya wanaCCM ambao wanakidharau chama na kukiona sio chochote, huku akitoa mfano wa kiongozi mmoja hivi karibuni aliyevuliwa uanachama kutokana na utovu wa nidhamu na kumtaka asijihusishe na shughuli zozote za chama.

Alisema mtu huyo alisahau mema yote aliyofanyiwa na chama ikiwamo kupewa madaraka makubwa hadi serikalini na kwamba bado aliendelea kukichafua chama.

"Kuna mambo nashindwa kuyaelewa yuko mtu mmoja hapa nchini amesoma na amepata kazi serikalini, amekuwa mwandamizi, baadaye CCM ikamwona anafaa kuwa kiongozi akahudumu kwa miaka takribani 10 ndani ya chama, alikuwa mshamba tu hata suti alikuwa hajui kuvaa, lakini tukampa suti za hapa na pale, tukampeleka ng'ambo, lakini akasahau kung'aa kwake kumetokana na chama, ukibeba adhabu kaa kimya acha kupiga mdomo, nawasihi vijana epukaneni na tabia na mienendo yao," alisema Polepole.

Alisema ni bora kiongozi huo akaendelea kukaa kimya kuliko kuongea maneno yasiyofaa, huku akisema ukimya ni jibu zuri licha ya kwamba watu wa namna hiyo wako na wataendelea kuwapo, licha ya kuwa uimara wa chama hicho uko katika nidhamu yake inakwenda sambamba na unyenyekevu.

Alisema Kamati Kuu ya CCM, ikishafanya uamuzi wa kumfukuza mtu uanachama aidha atake au asitake lazima atoke, ndio imeshatoka maana kamati hiyo inaundwa na watu makini na wenye maamuzi magumu akiwamo Mwenyekiti ambaye ni Rais Dk. John Magufuli, Philip Mangula, Dk. Bashiru Ally, na wengine.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema anatamani Jimbo la Mbeya mjini ambalo kwa sasa liko chini ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) lirudi mikononi mwa CCM kwa madai kuwa amechoka kuwaongoza watu wanaofanya vurugu.

Alisema chama pekee chenye amani ni CCM, hivyo anatamani kishinde na kuchukua jimbo hilo la Mbeya mjini huku akiwaomba wanaCCM kuendelea kushikamana na kuepuka mpasuko ambao unaweza kukigawa chama na kuwapa faida wapinzani.

# Wananchi wafurahia ujenzi barabara kufungua uchumi

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

WANANCHI wilayani Ileje, wamesema kukamilika kwa barabara ya Mpemba- Isongole inayojengwa na serikali kwa gharama ya Sh. bilioni 107.55 kutawezesha wilaya hiyo kufunguka kiuchumi na biashara.

Wakizungumza na gazeti hili jana, walisema wilaya hiyo ina rasilimali nyingi katika kilimo na biashara, lakini kikwazo kikubwa ni miundombinu ya usafirishaji.

Mmoja wa wananchi hao, Simion Mkondya, alisema wananchi wa Ileje ni wazalishaji wa mahindi, alizeti na karanga kwa wingi, lakini wameshindwa kupata tija kupitia kilimo kutokana na mazao yao kukosa ya uhakika wa kuuza kwa bei nzuri.

"Tunashukuru serikali kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa barabara yetu ya Mpemba - Isongole baada ya kusimama kwa muda...kwa kweli ikikamilika itafungua uchumi na biashara hapa Ileje, watu wanaweza kupeleka mazao yao hadi Dar es Salaam na kuyauza kwa bei nzuri tofauti na wakiuza hapa kwa walanguzi," alisema Mkondya.

Alisema, barabara hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kufanyika kwa biashara za mpakani kati yake na nchi jirani ya Malawi, hali itakayosaidia pia kuchangamka kwa biashara na kuongeza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na wilaya kwa ujumla, pamoja na kufanya miji ya Isongole na Itumba kukua kwa haraka.

Naye Lydia Songa, mchuuzi wa biashara ya mpakani alisema kwa sasa imekuwa ni vigumu kuwafikia wateja wao waliopo katika miji ya Mpemba, Vwawa na Mbeya kutokana na miundombinu kutoridhisha.

Kwa upande wake Mkuu wa wilaya hiyo, Joseph Mkude alisema ujenzi wa barabara hiyo ni sehemu ya ahadi ya Rais Dk. John Magufuli aliyoahidi wakati wa kampeni na utekelezaji wake umekamilika kwa asilimia 65 na gharama yake ni Sh. bilioni 107.55.

Alisema Rais Magufuli wakati wa kampeni za kuomba kura za urais mwaka 2015 akiwa Wilaya ya Ileje, aliahidi kuijenga barabara hiyo na alipochaguliwa kuwa rais alitimiza ahadi hiyo.

Alisema barabara hiyo ni kiungo muhimu kati ya Tanzania na Malawi katika sekta ya uchumi na biashara, lakini itarahisisha kazi za ulinzi na usalama.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Songwe, Yohani Kasaini, alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 50.3 inatarajiwa kukamilika Septemba 10, mwaka huu na wananchi kuanza kunufaika kwa kusafiri na kusafirisha bidhaa mbalimbali.

Alisema tayari wameshakamilisha madaraja manne yaliyopo katika maeneo ya Mbebe, Ikumbilo, Msiya na Isongole ambayo yalikuwa na changamoto kubwa kutengeneza kipindi cha mvua jambo lililosababisha mkandarasi kusubiri mvua zisimame.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## CHETI KIMEPOTEA



**EFESO RUBEN MGAYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Uwalimu Chenye Index **No.E0528/0360** Kilichotolewa na TANDALA **TEACHER'S COLLEGE** mwaka 2019..Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/458108/2020.**

115786902

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na: 37 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MAREHEMU JONATHAN RUGAIMUKAMU EZEKIEL**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**CECILIA KOKUKWEYENDERA EZEKIEL**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 23 mwezi wa Julai 2020.
Imewasilishwa Dar es Salaam, leo tarehe 1 mwezi wa Juni 2020.

.........................................

**NAIBU MSAJILI**
**NAKALA KWA:**
**MUTABUZI & CO. ADV.**
**NIC LIFE HOUSE**
**5TH FLOOR, WING B**
**P.O BOX 5539, DSM**

115786402

---

**MHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo:**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;165/2020**

**Ombi la FRANK JOHN SENKONDO**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu**
**MONICA FRANK SENKONDO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 30/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/06/2020.

115787602

---

## PLOTS FOR SALE IN DODOMA

LARGE SURVEYED PLOTS ARE AVAILABLE FOR IMMEDIATE SALE. IDEAL FOR LARGE BUSINESSMEN AND/OR LIVESTOCK KEEPERS. CALL AND/OR SEND MESSAGE THROUGH PHONE NO **0762840928.**

215787502

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RADIX TECHNOLOGY TANZANIA LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 853 DMM** aina ya **SUBARU FORESTER** rangi ya Grey, Engine namba **SH5004603.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/464795/2020.**

115787402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;157/2020**

**Ombi la PHILEMON BRIGHTON MWAKYUSA**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu**
**ANNA BRIGHTON MWAKYUSA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/06/2020.

115786702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 46/2020**

**Ombi la EMMANUEL ANDREW MSENGI**
**kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu**
**EBETHANI ZAKAYO MSENGI**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 25/6/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 4/6/2020

215786802

---

**FORM 11**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Uchira**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NO , 05 mwaka 2020**

**Ombi la NUHU HUSENI MSANGI**

**Usimamizi wa mirathi ya marehemu**
**HUSENI…….ABDARAMANI MSANGI WA**
**KAWAWA ROAD**

Watu wote mnaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa

Kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe ….30…/06/….2020………kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 12/06/2020

215786602

---


***Uza,***

***Chenye Thamani***

***Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Trump atangaza mwisho wa viza kwa wageni Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameongeza muda wa kusitishwa kwa viza za bahati nasibu, pamoja na zile za wafanyakazi wa kigeni, hadi mwishoni mwa mwaka huu.

Kutokana na agizo hilo, wafanyakazi wenye ujuzi mkubwa wa kiufundi, pamoja na ambao hawako katika sekta ya kilimo na maofisa wakuu wa kampuni wataathirika.

Taarifa kutoka Ikulu ya Marekani iliyotolewa jana ilieleza kuwa hatua hiyo itabuni ajira kwa Wamarekani wasio na kazi baada ya kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Lakini wakosoaji wanasema kwamba Ikulu ya Marekani inatumia janga la ugonjwa wa corona ili kukaza sheria za uhamiaji.

Katika mkutano na vyombo vya habari, Serikali ya Marekani imeeleza kuwa usitishwaji huo utawaathiri watu 525,000.

Watu hao ni pamoja na 170,000 waliozuiliwa na hatua ya kusitisha visa za bahati nasibu ambazo zinawapatia raia wa kigeni makazi ya kudumu nchini Marekani.

Ikulu ya Marekani kwa mara ya kwanza ilitangaza kuwa inasitisha viza hizo Aprili, mwaka huu.

Hata hivyo, raia wa Kigeni walio na viza kwa sasa hawataathirika kufuatia sheria hizo mpya zilizotangazwa siku ya Jumatatu.

Agizo hilo pia litawashirikisha wale walio na viza aina ya H-1B, ambazo nyingi hupewa wafanyakazi wa Kihindi ambao wana ujuzi wa kiufundi.

Mwaka uliopita, kulikuwa na takriban watu 225,000 waliotuma maombi wakishindania kazi 85,000 zilizopo kupitia mpango wa visa za H1-B.

Agizo hilo pia litawaathiri wale wanaotaka viza za muda mfupi aina ya J-1, orodha inayowashirikisha wanafunzi wa vyuo vikuu na mayaya.

Maprofesa na wasomi hawakushirikishwa katika agizo hilo.Kutakuwa na kifungu cha kuwaruhusu baadhi ya walioathiriwa iwapo watatuma maombi.

Visa za mameneja na wafanyakazi wengine muhimu wa kampuni ya kimataifa pia zitasitishwa.

***BBC***



Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Urusi, Sergei Ryabkov, akiwasili katika ukumbi wa mazungumzo kuhusu mkataba wa New Start mjini Vienna. **PICHA: REUTERS**

# Marekani, Urusi zajadili mkataba wa nyuklia

**Vienna, AUSTRIA**

WAJUMBE wa Marekani na Urusi wanajadiliana mjini Vienna kuhusu mkataba wa silaha za nyuklia.

Mataifa hayo yamekutana wakati ambapo mvutano ukiongezeka baina yao, yanaona thamani katika kudhibiti umiliki wa silaha.

Rais wa Marekani Donald Trump anashikilia msimamo wake kwamba China inapaswa kushirikishwa kwenye mazungumzo hayo ambayo yamejikita katika kudhibiti umiliki wa vichwa vya nyuklia.

Marekani imekuwa ikidai kuwa China imekuwa na uhuru wa kufanya itakavyo kutengeneza mifumo ya silaha.

China kwa upande wake imeonyesha kutokuwa na nia ya kujiunga kwenye mazungumzo hayo, na hivyo kuzusha lawama kutoka Marekani.

Hata hivyo, wachambuzi wanahoji kuwa Marekani inauona msimamo wa China kama fimbo muhimu ya kukabiliana na uhasama unaoendelea kukua dhidi yake.

Ujumbe kwenye mazungumzo hayo haukutoa taarifa yoyote ulipowasili katika ukumbi wa mkutano.

Mjumbe maalum wa Marekani katika mazungumzo hayo, Marshall Billingslea, alituma picha kwenye ukurasa wa mtandao wa Twitter ikionyesha viti vitupu na bendera ya China kwenye mazungumzo hayo, pamoja na maelezo kuwa China haipo kwenye mazungumzo. Hatua ambayo imeshutumiwa na China ikisema hawakuwa wamepanga kushiriki mazungumzo hayo.

Billingslea alisema China bado inajificha nyuma ya ukuta mkubwa wa siri kuhusu utengenezaji wake wa silaha za nyuklia na mambo mengine mengi.

Mkurugenzi Mkuu wa chama cha kudhibiti umiliki wa zana za kivita, chenye makao yake makuu mjini Washington, Daryl Kimball, alisema msisitizo wa kuishirikisha China kwenye mazungumzo hayo unaonyesha utawala wa Rais Trump hauzingatii kikamilifu utekelezwaji wa mkataba huo.

**DW**

# Kifungo cha Vital Kamerhe chazua gumzo DRC

**KINSHASA, DRC**

GUMZO limezuka kila kona katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) baada ya mwanasiasa, Vital Mamerhe, kufungwa miaka 20 jela baada ya kupatikana na makosa ya kufuja fedha za umma.

Katika Jiji la Bukavu na katika maeneo mengi ya mkoa Kivu Kusini, ambako Vital Kamerhe anatokea mijadala imekuwa mikali kuhusu kufungwa kwa mwanasiasa huyo.

Vital Kamerhe anashtumiwa kutumia vibaya zaidi ya dola milioni 50 za Kimarekani zilizokuwa zimetengwa kugharamia ujenzi wa makazi ya polisi na maofisa wa jeshi jijini Kinshasa.

Kamerhe alikuwa Mkurugenzi katika Ofisi ya Rais, kabla ya kuakamatwa kwake na kushtakiwa.

Jaji Pierrot Bakenge, aliitangaza hukumu ya kifungo cha miaka 20 dhidi ya Kamerhe kwa kesi ya ufisadi ambayo ilikuwa inamkabili.

Hukumu ambayo hadi sasa chama chake wameendelea kutupiliwa mbali wakisema kuwa kesi hiyo ni ya kisiasa ambayo inalenga kumtenga kiongozi wao katika siasa za DRC.

"Hatutakubali kiongozi wetu afungwe kwa vitu ambavyo hakufanya. UNC tumeelewa kwamba madai yote haya yanalenga kumpaka tope ili asiwe mgombea kwa uchaguzi wa mwaka 2023," alisema Sele Yemba, msemaji wa chama UNC.

Hata hivyo, Chama cha UDPS mshirika wa chama cha Kamerhe kimesema, hatua hio haiwezi kuvunja uhusiano wao.

"Chama cha UDPS tumesema kuwa, ndugu zetu wa UNC tuko pamoja, kwani yule ambae amefungwa ni Kamerhe lakini UNC iko, tutaendelea kushirikiana pamoja, UDPS na UNC ni muungano mmoja," alisema Aldolphe Amisi, msemaji wa chama cha UDPS cha Rais Felix Tshisekedi.

Hii ni mara ya kwanza katika historia ya DRC kuona Ofisa Mwandamizi akihukumiwa na kufungwa jela akiwa anatekeleza majukumu yake serikalini.

**RFI**

# Ripoti: Robo milioni ya watoto duniani wakosa elimu

**PARIS, Ufaransa**

RIPOTI mpya ya hali ya elimu duniani ya shirika la Umoja wa Mataifa la elimu, sayansi na utamaduni (Unesco) imeonesha kuwa karibu watoto milioni 258 hawakwenda shule mnamo mwaka 2018.

Imesema idadi hiyo ni sawa na asilimia 17 ya vijana ulimwenguni kote.

Kulingana na makadirio Shirika hilo, takriban asilimia 90 ya vijana walioathiriwa zaidi ni kutoka katika nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia. Umasikini umetajwa kuwa ndiyo haswa unaoathiri fursa za elimu.

Ripoti hiyo pia imeeleza kwamba mamilioni ya wavulana na wasichana wanabaguliwa katika mifumo ya elimu kwa sababu ya asili zao au ulemavu walionao.

Mkurugenzi Mkuu wa Unesco, Audrey Azoulay, alisema janga la corona limeathiri zaidi shughuli za elimu na kwamba tatizo hilo la kiafya linaweza kuwa chanzo cha kuwafanya watoto wengi wasirudi shuleni hasa wasichana kutoka familia masikini.

Alisema nchi nyingi bado zina matendo ya kuwabagua watoto kimasomo, ambayo yanachochea uhasama, ubaguzi na kutengwa.

Alisema ni nchi 41 tu ulimwenguni zinazotambua rasmi lugha ya ishara na kote ulimwenguni, shule nyingi zinang'ang'a pakubwa ya kuweza kupata huduma za mtandao kuliko kuwapa kipaumbele wanafunzi wenye ulemavu.

Azoulay alisema ili kuondokana na changamoto hii hoja ya kuwekeza elimu kwa kuwajumuisha wote bila ubaguzi ni muhimu zaidi na kwamba kushindwa kuchukua hatua endelevu ni kitendo kitakachozuia maendeleo kwa jamii.

Ripoti hiyo ya pia imebaini kuwa katika nchi zenye kipato cha chini na cha kati, watoto wenye ulemavu, kwa asilimia 19 wapo chini ya kiwango cha kuhudhuria masomo na kwamba katika mataifa 20 masikini, barani Afrika yaliyo Kusini mwa Jangwa la Sahara, wengi wa wasichana wa vijijini hawapati elimu ya shule ya sekondari.

***DW***

## HABARI MICHEZO



# MOURINHO
## AJITETEA TUHUMA ZA KUUA VIPAJI

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amemjibu mchezaji wa zamani wa Arsenal, Paul Merson, ambaye alisema raia huyo wa Ureno amekua sababu ya kuharibu vipaji vya wachezaji.

Mourinho amejibu tuhuma hizo, baada ya kikosi cha Spurs kuambulia matokeo ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Manchester United mwishoni mwa wiki, ambapo mshambuliaji, Harry Kane hakuonyesha makali yake kama alivyokuwa chini ya Mauricio Pochettino.

Katika mchezo huo Kane aligusa mipira mara 36 tu na kufanikiwa kupiga shuti moja lililolenga lango la wapinzani, mlinda mlango Hugo Lloris ndiye aliyegusa mara chache zaidi ya mshambuliaji huyo kutoka England, ambaye tayari ameshazifumania nyavu mara 11 msimu huu.

"Nafikiri Kane hana shida ya kufunga kwenye kikosi changu, hasa anapokuwa fiti asilimia 100," alisema Jose Mourinho.

"Ulikuwa mchezo ambao Manchester United walipata nafasi nyingi, ndiyo maana mshambuliaji wao Anthony Martial alipata nafasi, lakini Kane angepata zile angefunga bila shida" aliongeza.

Wakati akitetea tuhuma za kuwaharibu washambuliaji, Mourinho ametaja orodha ya washambuliaji ambao alifanya nao kazi na wakatwaa viatu vya dhahabu vya ufungaji bora kama Didier Drogba, Cristiano Ronaldo na Zlatan Ibrahimovic ambaye alifanya nae kazi Manchester United na Inter Milan.

"Nina idadi nzuri ya washambuliaji ambao walifanya kazi nzuri chini yangu," alisema.

## SOLSKAJAER ASIFIA KIWANGO CHA POGBA

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskajaer amesema kiungo, Paul Pogba ni miongoni mwa wachezaji bora duniani kutokana na uwezo wake ndani ya uwanja akiwa pale Manchester United.

Pogba, mwenye umri wa miaka 27 aliwashangaza wengi kwa kuonyesha uwezo mkubwa kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Tottenham kwa kutimiza majukumu yake vema na kuhusika kwenye pointi moja ambayo United waliipata wakati wakilazimisha sare ya kufungana bao 1-1.

Akitokea benchi dakika ya 63 kwenye mchezo huo wakati United ikiwa imefungwa bao 1-0, bao hilo lilifungwa na Steven Bergwijn dakika ya 27, ambapo United walisawazisha dakika ya 81 kwa mkwaju wa penalti uliopigwa na Bruno Fernandes.

Penalti hiyo ilisababishwa na Pogba baada ya kuchezewa faulo ndani eneo la hatari na Eric Dier, sare hiyo inawafanya United wafikishe jumla ya pointi 46 wakiwa nafasi ya tano huku Tottenham ikifikisha pointi 42 nafasi ya nane na zote zimecheza mechi 30.

"Kipindi cha pili kwa namna ambavyo tumecheza tulistahili kupata pointi tatu, lakini hakuna tatizo tumeanza vizuri, wachezaji wangu wamecheza vizuri, Pogba amefanya makubwa na ni mchezaji bora ndani ya ulimwengu kwa sasa kwa kuwa ana vitu vingi," amesema.

Pogba hakuwa uwanjani kwa muda mrefu tangu Desemba mwaka jana ambapo alikuwa akisumbuliwa na majeraha.



## NEYMAR ALITAKA TAJI LA UEFA

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ametuma ujumbe kwa wapinzani wa Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu kwamba, wajipange kwa sababu amedhamiria kuandika historia mpya.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil, anataka kuisaidia klabu yake kushinda taji hilo la ubingwa wa Ulaya, ikiwa hawajaonja utamu wa kulibeba kwa kipindi cha miaka 49. Na sasa amedai PSG imedhamiria kubeba ubingwa huo msimu huu.


Neymar, amekuwa mchezaji ghali zaidi duniani wakati aliponaswa na PSG kwa mkwanja wa pauni milioni 198, ambao umeongezeka na kufika pauni milioni 201 mwaka 2017.

Na sasa akiwa kwenye kiwango bora na kujikusanyia wachezaji baada ya msimu huu kufunga mabao 13 katika mechi 15 alizocheza kwenye Ligue 1, Neymar mpango wake mkuu ni kuipa PSG ubingwa wa Ulaya na baada ya hapo atafungua milango ya kutimkia kwingineko.

Fowadi huyo alifunga mara mbili PSG ilipoisukuma nje Borussia Dortmund kwa jumla ya mabao 3-2 katika hatua ya mtoano ya 16 bora kwenye michuano hiyo msimu huu kabla haijasimamishwa kutokana na janga la corona.

Neymar alisema: "Sasa nipo vizuri na ninachokifikiria ni Ligi ya Mabingwa Ulaya tu. Tuna kikosi imara na tumefuzu kibabe, hivyo tunasubiri tu shughuli ianze, nimekumbuka sana. Nasubiri kwa hamu kuingia uwanjani na kwa mapenzi ya Mungu, tutaandika historia."

Uefa imepanga michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu kwa kuanzia hatua ya robo fainali ifanyike katika nchi moja, huko Ureno kutokana na kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona. Kwenye hatua hiyo, itacheza mechi moja tu na si mbili kama ambavyo ilivyokuwa kawaida yake.






## ARTETA AMWANIA BEKI PSG

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ameingia kwenye mbio moja na Chelsea kumwania mlinzi wa kushoto wa Paris Saint-Germain, Layvin Kurzawa, ambaye atakuwa mchezaji huru wakati wa dirisha lijalo la usajili wa majira ya joto.

Kocha huyo raia wa Hispania yupo sokoni kunasa wachezaji wa gharama nafuu baada ya timu hiyo bajeti yake ya usajili kubana kutokana na janga la mlipuko wa virusi vya corona.

Chelsea wao wamekuwa wakimtolea macho Kurzawa, wakiamini ni chaguo mbadala kwenye mpango wao wa kunasa huduma ya Ben Chilwell kama watashindwa kumsajili kutoka Leicester City.



Kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers anaamini Chilwell atabakia kwenye kikosi chake wakati wa dirisha la mwaka huu la uhamisho wa majira ya joto.

Marcos Alonso na Emerson wameshindwa kufanya mambo na kumfanya Frank Lampard kumwambia mkurugenzi anayeshughulikia usajili huko Stamford Bridge, Marina Granovskaia kumletea mabeki wapya wa pembeni.

Kurzawa, aliwahi kuichezea Monaco na yupo kwenye kikosi cha PSG tangu msimu wa 2015/16, akicheza jumla ya mechi 123 kwenye kikosi hicho na kubeba mataji matatu ya Ligue 1, matatu ya Kombe la Ufaransa na mengine kibao, huku mkataba wake ukimalizika mwisho wa msimu.

## NYOTA WAPYA WAMPAGAWISHA LAMPARD

**LONDON, England**

FRANK Lampard amekiri ana presha kwa sasa namna atakavyopanga kikosi chake msimu ujao baada ya usajili wa Timo Werner na Hakim Ziyech.

Chelsea iliyoshindwa kusajili kwenye dirisha la majira ya joto mwaka jana kutokana na kufungiwa, imewasajili wachezaji wawili kwa ajili ya kuimarisha safu ya ushambuliaji.

Baada ya timu kuwa na adhabu ya kusajili, Lampard, aliyerithi kikosi hicho kutoka kwa Maurizio Sarri mwaka jana, alitoa nafasi kwa makinda kucheza msimu huu kabla ya kuingia sokoni kuleta sura mpya.

Kikosi hicho kinachoripotiwa kuwasaka Kai Havertz na Ben Chilwell, msimu huu kimekuwa kikitegemea zaidi huduma ya makinda Mason Mount, Tammy Abraham na Reece James wakipambana kuhakikisha timu inamaliza msimu wa ligi ndani ya nne bora ili kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Tangu adhabu imalizike, Chelsea imetumia pauni milioni 48 kunasa huduma ya Werner na pauni milioni 38 kumsajili Ziyech raia wa Morocco.

Kikosi hicho cha Stamford Bridge kitaachana na wakali wake Willian na Pedro mwishoni mwa msimu na Lampard alisema: "Presha siku zote zimekuwa juu kwa sababu tunatumia pesa. Lakini, kazi hii siku zote ni ya presha.

"Tunajaribu kuboresha kikosi. Hilo litanifanya kuwa na presha zaidi."

## MESSI, GRIEZMANN NUSURA WAZICHAPE

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi na Antoine Griezmann wameripotiwa kutibuana mazoezini na kumfanya kocha wao Quique Setien kuingilia kati kuweka mambo sawa.

Griezmann ameshindwa kuonyesha kiwango bora tangu alipotua Barcelona kwa ada ya pauni milioni 108 akitokea Atletico Madrid kwenye dirisha la majira ya joto mwaka jana.

Na Barcelona kwa sasa inatazama namna ya kupunguza bili ya mishahara kwenye kikosi chao baada ya janga la virusi vya corona, huku hesabu zikipigwa za kumuuza nyota huyo wa Ufaransa.

Manchester United walihusishwa juu ya kumsajili fowadi huyo kabla ya kwenda kujiunga na Barcelona, huku kinachosemwa ni kwamba miamba hiyo ya Old Trafford inaweza kuihitaji tena saini yake kama wakisikia amewekwa sokoni.

Taarifa iliyoripotiwa na tovuti ya Diario Gol ya huko Hispania imedai kwamba Messi na Griezmann walitibuana kwenye mazoezi ya timu hiyo na kumfanya kocha wao Setien na wachezaji wengine wa timu hiyo kuingilia kati kuweka mambo sawa ili wasirushiane ngumi.

Katika mechi dhidi ya Leganes, Messi aliripotiwa kutompasia mchezaji mwenzake huyo hata mara moja.

Na sasa wakati Griezmann akionekana kwamba atafunguliwa mlango wa kutokea, Messi anaripotiwa kukaribia kusaini dili jipya litakalomfanya kuendelea kubaki Nou Camp kwa muda mrefu zaidi.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BELLINGHAM AKARIBIA KUSAJILIWA DORTMUND

Inaelezwa kinda huyo atasaini mkataba wa miaka minne na vigogo hao wa Bundesliga...

**DORTMUND, Ujerumani**

BORUSSIA Dortmund imekaribia kunasa saini ya mshambuliaji ghali chipukizi wa Birmingham, Jude Bellingham.

Klabu hiyo inayoshiriki Bundesliga, ambayo pia ilisaidia kwa kiasi kikubwa kukuza kipaji cha Jadon Sancho, inakaribia kutangaza kuingia mkataba na nyota huyo ndani ya siku chache, huku Dortmund ikiweka wazi iko tayari kulipa ada ya pauni milioni 18 ili kukamilisha mchakato huo.

Manchester United inajulikana kuwa kwenye mbio za kumwania mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 16, na iliamua kumwalika kutembelea katika viwanja vya mazoezi, lakini inaonekana kushindwa kufanikisha mchakato huo.

Klabu mbalimbali za Ulaya zilionyesha kuvutiwa na kinda huyo, lakini mwenye ameonekana anataka kukamilisha mazungumzo ya kujiunga na Dortmund.

Bellingham ataruhusiwa kusaini mkataba kama mchezaji wa kulipwa atakapofikisha umri wa miaka 17, ifikapo Juni, 29 mwaka huu.

Kwa sasa mchezaji huyo analipwa pauni 145 kwa wiki katika klabu hiyo ya Birmingham, lakini inaelezwa ofa yake mpya atakuwa analipwa pauni 60,000 kwa wiki.

Akiwa ni mchezaji ambaye amecheza kwa kujituma na kwa uaminifu kwenye klabu hiyo ya St Andrew, nyota huyo anatarajia kukamilisha msimu kabla ya kupanda ndege kwenda Ujerumani.

Taarifa zinaonyesha tayari makubaliano yameshafikiwa kama ilivyokuwa kwa nyota wa Timu ya Taifa ya England, Sancho aliyetoka Manchester City na kujiunga na Dortmund mwaka 2018 kwa dau la pauni milioni 6.3.

Kwa mujibu wa ESPN, Dortmund imekuwa ikimfuatilia Bellingham tangu mwaka msimu wa 2018/19, sasa wamefanikiwa kumnasa huku wakimwahidi watamfanya kuwa mchezaji wa kiwango cha juu.

Lakini inaonyesha maofisa wa Old Trafford wataumia kumkosa mchezaji huyo mwingine ambaye alikuwa katika mipango yao.

Dortmund pia ilifanikiwa kunasa saini ya Erling Haaland katika dirisha la majira ya baridi ambaye alikuwa pia anawaniwa na United.

Bellingham ameichezea Birmingham mechi 33 na hivi karibuni alikuwamo kwenye kikosi kilichowavaa mahasimu wao wa mji wa Midlands, timu ya West Brom hapo Jumamosi.

Amefunga mabao manne na kutoa pasi tatu za mwisho msimu huu.

## KWA UFUPI

**HENDERSON AITEGA UNITED**

GOLIKIPA wa Manchester United, Dean Henderson (23), ambaye yuko kwa mkopo Sheffield United, atasaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Old Trafford kama atahakikishiwa kuwa mlinda mlango namba moja. Chelsea na Tottenham pia zinamwania golikipa huyo raia wa England. ***(Manchester Evening News)***

**PSG YAMKUBALI KURZAWA**

PARIS St-Germain imempa ofa ya kusaini mkataba mpya wa miaka minne beki wake wa kushoto Mfaransa, Layvin Kurzawa (27), ili kumaliza uvumi wa kuhusishwa na mipango ya kujiunga na Arsenal na Chelsea. ***(France Football - in French)***

**KURZAWA KUMRITHI HENRIQUE**

ATLETICO Madrid inajiandaa kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Layvin Kurzawa ili kuchukua mikoba ya Mbrazil, Caio Henrique ambaye ana umri wa miaka 22 na anajiandaa kujiunga na Porto. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**MEUNIER RASMI DORTMUND**

BEKI wa kulia wa Ubelgiji, Thomas Meunier atajiunga na Borussia Dortmund akitokea Paris St-Germain akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni wa mwezi huu. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 amesaini mkataba wa miaka minne na klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Bild - in German)***

**CAVANI AIKATALIA PSG**

STRAIKA wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani (33), hatasaini mkataba mfupi wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo ili kuichezea kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa sababu anaondoka katika klabu hiyo inayoshiriki Ligue 1 mwezi huu. ***(RMC Sport - in French)***

**AJAX YAMLILIA ONANA**

MASHABIKI wa Ajax walionekana Jumatatu wiki hii wakiwa wamebandika bango kwenye uwanja wa mazoezi wa klabu hiyo lenye ujumbe wa kumshawishi golikipa wao Mcameroon, Andre Onana (24), abakie licha ya kutakiwa na Barcelona, Chelsea na Tottenham. ***(Mail)***

**MKHITARYAN, KLUIVERT KUBADILISHANA**

WAKALA Mino Raiola yuko katika mazungumzo na Arsenal pamoja na Roma ili kujadili uwezekano wa kiungo, Henrikh Mkhitaryan (31), na winga wa Timu ya Taifa Uholanzi, Justin Kluivert (21), kubadilishana klabu. Kwa sasa Mkhitaryan yuko kwa mkopo katika klabu hiyo ya Italia akitokea The Gunners. ***(Calciomercato - in Italian)***

**ARSENAL NJIA PANDA**

ARSENAL inatakiwa kufanya uamuzi kuhusiana na hatima ya beki wake wa kati Mbrazil, David Luiz (33), Mhispania Pablo Mari (26), Mreno, Cedric Soares (28), na kiungo Mhispania, Dani Ceballos (23), ifikapo Jumanne baada ya kumalizika kwa mikataba yao. ***(Sun)***

**PASALIC AONDOKA CHELSEA**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Croatia, Mario Pasalic (25), amejiunga na Atalanta inayoshiriki Serie A kwa mkataba wa kudumu baada ya kukaa Chelsea kwa muda wa miaka sita bila ya kucheza hata mechi moja. ***(Sky Sports)***

**RODGERS AMTAKA CHILWELL**

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers amezionya klabu kubwa ambazo zinamwania nyota wake, Bel Chilwell na kueleza Foxes inapambana kumbakisha beki huyo. ***(Mail)***

**O'HARE MAMBO SAFI**

MABOSI wa Coventry City wako tayari kumpa mkataba wa kudumu kiungo wa Aston Villa, Callum O'Hare wiki hii. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 amedumu kwa mkopo na mwaka mmoja na klabu hiyo. ***(Coventry Telegraph)***

HABARI MICHEZO

# ALLIANCE FC YAJIKOMBOA KATIKA 'GUNDU' LA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa bao 1-0 iliopata Alliance FC dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya Jumamosi iliyopita, umeondoa 'mkosi' kwa timu hiyo baada ya kupokea vipigo vitano mfululizo kabla ya mechi hiyo.

Ikiwa ugenini, Alliance FC yenye maskani yake jijini Mwanza, ilishinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na Juma Nyangi na kuondoa 'jinamizi' la kutoshinda mechi tano mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tangu ilipofungwa na Yanga mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Februari 29, mwaka huu, Alliance ilikuwa ni kama imeachiwa 'gundu' kwani ilipokea vipigo mfululizo.

Kabla ya kufungwa na Yanga, Alliance ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida United ikiwa nyumbani katika mchezo uliofanyika Februari 23, mwaka huu.

Baada ya kuchapwa na Yanga, Alliance ilipokea kipigo cha pili cha bao 1-0 kutoka kwa Ruvu Shooting Machi 4, mwaka huu kabla ya kufungwa tena bao 1-0 Machi 7, mwaka huu dhidi ya Azam FC.

Mkosi uliendelea kuiandama Alliance, ambapo Machi 11, mwaka huu ilidungwa bao 1-0 dhidi ya Prisons, na mechi ya tano ilikuwa siku mbili kabla ya Ligi Kuu kusimamishwa kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19, na Machi 15, mwaka huu ilipobamizwa mabao 2-1 dhidi ya KMC.

Pamoja na ushindi hiyo, timu hiyo bado ina kazi ya kufanya, kwani inakamata nafasi ya 17 ikiwa na pointi 32 kwa michezo 30 ambayo imecheza, ikibakisha mechi nane tu kumaliza msimu huu wa 2019/20.

Leo timu hiyo inatarajiwa kushuka dimbani kucheza dhidi ya Polisi Tanzania, ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Nyamagana.




Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael (kushoto), akitoa maelekezo kwa beki wa timu hiyo, Juma Makapu, katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC, iliyochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Ihefu yaendelea 'kuiota' Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ihefu FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza umesema umejipanga kushirikiana 'bega kwa bega' na benchi la ufundi pamoja na wachezaji wao, kuhakikisha timu hiyo inashinda mechi zilizobakia na hatimaye kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Fred Chalamila, alisema mipango yao ni kuhakikisha wanafanya vema katika kila michezo inayowakabili bila kujali mpinzani wanayekutana naye.

Chalamila alisema kwa sasa wanaendelea kujiimarisha ili waibuke na ushindi katika mechi yao dhidi ya African Lyon itakayochezwa Jumamosi.

"Tumezungumza na benchi la ufundi, kwa kiufundi wamejipanga vizuri kuhakikisha tunashinda mechi zetu, wanaboresha pia safu ya ushambuliaji ili kupata idadi nzuri ya mabao katika kila mechi," alisema Chalamila.

Katibu huyo alisema wachezaji wote wana ari kwa sababu ndoto zao ni kukata tiketi ya kucheza Ligi Kuu Bara.

"Hatuifuatilii Dodoma FC, maana wao pia wamejipanga kufanya vizuri, hivyo ni jukumu letu nasi kuhakikisha tunashinda mechi zetu bila kuwaangalia wapinzani wetu," Chalamila alisema.

Ihefu yenye pointi 42 sawa na kinara wa Kundi A, Dodoma FC ambayo yenyewe ina wastani mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa.

## Kombe la Nyerere kufanyika Oktoba

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Magongo Tanzania (THA), kimetangaza mashindano ya Kombe la Nyerere yatakayofanyika Oktoba, mwaka huu huko Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Mashindano hayo yanatarajiwa kushirikisha timu za mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Kaushik Doshi, alisema wachezaji wote wanaendelea vema na mazoezi kwa ajili ya kuonyesha ushindani katika mashindano hayo.

"Wachezaji wapo vizuri na kila siku wanajinoa kuhakikisha wanazidi kujiimarisha na kupandisha viwango vyao," alisema Doshi.

Katibu huyo alisema ugonjwa wa corona uliwaharibia mipango, lakini wanaamini kila mchezaji ataongeza juhudi ili kurejea kwenye ubora baada ya kukaa muda mrefu bila kushiriki mashindano yoyote.

"Ugonjwa wa corona umetuvurugia mipango mingi, tulilazimika kusimamisha kila kitu, naamini sasa hivi mambo yatarejea katika mstari na ushindani utaonekana," Doshi alisema.

Aliitaka mikoa kuandaa vema timu zake na hivi karibuni watatangaza tarehe rasmi ya kuanza kwa michuano hiyo.

## Michuano ya FA Zanzibar hatihati

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema bado hatima ya kurejea kwa mashindano ya Kombe la FA iko mikononi mwa serikali, imeelezwa.

Michuano hiyo ndio hutoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahmada Vuai, alisema ruhusa pekee waliyonayo ni ya kuendesha Ligi Kuu Zanzibar na uamuzi wa kuanza kwa Kombe la FA ambao unasubiri ridhaa ya serikali.

Alisema michezo mingine ambayo bado inasubiri ruhusa ya serikali ni pamoja na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, Kanda ya Pemba na Ligi ya Vijana.

"Bado hatuwezi kusema chochote kuhusu Kombe la FA kwa sasa, kwa kifupi itaendelea kusubiri hadi hapo serikali itakapotoka ruhusa ya kuendelea," alisema Vuai.

Kombe la FA lilikuwa limefikia hatua ya robo fainali kwa upande wa Kanda ya Unguja huku Kanda ya Pemba ilikuwa imefikia hatua ya 16 bora, ambapo washindi wa kila upande watakutana kusaka bingwa wa michuano hiyo.

Michezo
Jumatano Juni 24, 2020
Nipashe



## Bellingham akaribia kusajiliwa Dortmund
HABARI UK 22



Wachezaji wa Simba kutoka kushoto, Muzamiru Yassin, Rashid Juma (jezi namba 16) na Said Ndemla, wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo wakijiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbeya City itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya. **PICHA: RABI HUBE**

## SAFARI YA MOLINGA YANGA YAKAMILIKA

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kuwa kinara wa kupachika mabao ndani ya Yanga msimu huu, imeelezwa mshambuliaji, David Molinga, hana nafasi ya kuendelea kukitumikia kikosi hicho katika msimu ujao.

Hata hivyo Molinga na mshambuliaji mwenzake wa kimataifa, Yikpe Gislain, wamekuwa wakipigiwa kelele na mashabiki wa timu hiyo ambao hawaridhiki na viwango vyao.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema baada ya kumalizika kwa msimu huu, Molinga ataondoka moja kwa moja kwa sababu amekuwa haelewani na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo.

Chanzo hicho kilisema klabu haina mpango wa kumwongezea mkataba Mkongomani huyo na tayari ameshaelezwa.

"Tayari safari yake imewadia na mkataba wake unaisha msimu huu unapokamilika, hatakuwa ndani ya kikosi msimu ujao," kilisema chanzo chetu.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kwa sasa ni mapema kusema chochote kwa sababu sio wakati wa usajili.

# SIMBA SC, YANGA MAJARIBUNI BARA

Ni katika vita nyingine ya kusaka pointi tatu muhimu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imeingia ...

**Saada Akida na Grace Mwakalinga, MBEYA**

SAFARI ya kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena leo katika viwanja vitano nchini ambapo Yanga itawakaribisha Namungo kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam huku Mbeya City ikiwavaa vinara, Simba kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

Simba inayoongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 75, inahitaji kuvuna pointi tatu muhimu ili kukamilisha kampeni yake ya kutetea taji hilo, wakati Yanga yenyewe inataka kujihakikishia nafasi ya pili, ambayo pia inawaniwa na timu nyingine, ikiwamo Azam FC.

Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, alisema jana jijini kikosi chake kimejipanga vema kuhakikisha wanashinda mechi ya leo ili malengo yao yatimie.

Eymael alisema anafahamu Namungo ni moja ya timu zenye kutoka ushindani, lakini anaamini uzoefu wa wachezaji wake, utasaidia kuondoka na pointi tatu muhimu.

Kocha huyo alisema wamejipanga kutumia vema uwanja huo wa nyumbani na ushindi katika mchezo huo, utawaongezea morali ya kufanya vizuri kwenye mechi zinazofuata ikiwamo ya Kombe la FA itakayochezwa wiki ijayo.

Kiungo wa kimataifa wa Yanga, Haruna Niyonzima, aliiambia gazeti hili kila mechi iliyobakia kwao msimu huu ni sawa na fainali na kila mchezaji amejipanga kuonyesha kiwango bora.

"Tuna mechi ngumu, tunalijua hilo, kila timu inapambana hasa ukizingatia ni hatua ya lala salama, kwa upande wetu sisi Yanga ni kutopoteza mechi, malengo yetu ni kushinda tu, hatutaki kumaliza tukiwa nafasi ya tatu, tunahitaji nafasi ya pili," alisema Niyonzima.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, alisema kikosi chake kinaahidi kuwapa furaha mashabiki wa timu hiyo walioko Mbeya kwa kutangaza ubingwa wakiwa jijini humo.

Sven alisema wamejiandaa vyema kukabiliana na ushindani katika mechi ya leo ambayo wanafahamu wenyeji wao pia wanahitaji ushindi ili kujiondoa na janga la kushuka daraja.

"Wachezaji wangu wako vizuri na tumejipanga kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo yote miwili, tunataka kutangazia ubingwa tukiwa hapa Mbeya," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Meneja wa Uwanja wa Sokoine, Modestus Mwaluka, alisema wamejitahidi kuchukua tahadhari zote muhimu katika kukabiliana na ugonjwa wa corona kama ilivyoelekezwa na wataalamu wa afya.

Mecky Maxime, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, aliliambia gazeti hili 'hasira' zake za kupoteza mechi iliyopita dhidi ya Namungo atazihamishia katika mchezo dhidi ya Azam FC, utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Kaitaba, mjini Bukoba.

Maxime alisema kikosi chake kimejiandaa kurekebisha makosa yaliyotokea katika mechi dhidi ya Namungo na wataingia uwanjani kwa tahadhari.

"Tumesahau matokeo yaliyopita na kufanyia kazi upungufu, sasa kikosi kipo vizuri, pointi 41 tulizonazo si salama, kwa sababu klabu nyingine za chini zinaweza kutufikia na hivyo hatutaki kujiweka kwenye hatari ya kushuka daraja," alisema Maxime.

Naye Kocha Mkuu wa Azam, Aristica Cioaba, aliliambia gazeti hili amefanyia kazi upungufu uliyojitokeza katika mchezo wao uliopita na sasa wanapambana kuhakikisha wanavuna pointi tatu katika mechi ya leo.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni Alliance FC dhidi ya Polisi Tanzania wakati Biashara United itawakaribisha KMC FC kutoka Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >